# MATUMIZI YA TASWIRA KAMA KIGEZO CHA KUFANIKISHA MAUDHUI KATIKA *UTENDI WA SIIRAJI* ULIYOTUNGWA NA MUHAMMADI KIJUMWA


NA

DADSON M. NGUNJIRI

C50/61292/2010


TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI (M.A) KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI, IDARA YA ISIMU NA LUGHA

OKTOBA, 2012


University of NAIROBI Library

0389671 9

**UNGAMO**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe, na haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada Katika Chuo Kikuu Kingine.

………………………………… 31/10/12…………………………

**Sahihi** Tarehe:

**Dadson M. Ngunjiri**

**(Mtahiniwa)**

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi waliotelewa na chuo kikuu cha Nairobi.

………………………………… 2/11/2012…………………………

Sahihi: Tarehe:

**Dkt. Tom Mboya Olali.**

**(Msimamizi)**

………………………………… 2/11/2012…………………………

Sahihi: Tarehe:

**Dkt. Mwangangi wa Musyoka**

**(Msimamizi)**

# TABARUKU

Tasnifu hii naitabarukia kwanza kabisa Marehemu baba yangu aliyenipa dira ya taaluma na taadhima ya usomi, kwa mama yangu Rhoda aliyenilea, bibi yangu Geraldaine ambaye kila wakati alinipa moyo wa kuendelea na kazi yangu ya utafiti, na mwishowe watoto wangu Isaka, Rhoda na Kitinda mimba changu El-Daad kwa kunipa mutisha wa kuendeleza masomo yangu daraja kama hili.

# SHUKRANI

Kazi hii kwa hakika ingawa nimeishughulikia mie mwenyewe, ni vyema kusema kuwa imechangiwa na watu mbalimbali, kwani kidole kimoja hakiui chawa.

Mwanzo kabisa ninamshukuru Rabana kwa kunipa siha njema, na hekima iliyoniongoza, katika uwanja huu wa kiusomi na neema ambazo amenitunuku zimekuwa kawi kwangu na kuniwezesha kuitimiza ndoto yangu ya miaka mingi tangu utotoni, kupata shahada ya uzahimili katika somo la Kiswahili. Lugha mojawapo ya kitaifa na kimataifa. Ninakosa msamiati wa kuelezea yaliyoko moyoni walakini nitamsujudu, kweli nitatumikia duniani.

Shukrani zingine nazitolea wasimamizi wangu; Dkt. Tom M. Olali na Dkt. Mwangangi wa Mutiso kwa kunielekeza hatua kwa hatua na subira nyingi wazozisheheni hasaa pale ambapo chombo changu kilienda mrama wao ndio watia juhudi za kunielekeza na kunishauri ili kazi hii iwe ya kutamanika.

Shukrani zingine zimwendee Dkt. Kineene wa Mutiso kwa kunipa mwangaza katika utafiti wangu, Dkt. Iribe Mwangi, Dkt. Z. Ombogo, walionifunza wote nawapa Shukrani kwa kunipa nuru katika masuala ya kitaaluma.

Familia yangu kwa njia moja au nyingine hasaa bibi yangu Gathoni wa Kahinga aliweza kunipa ushauri wa kiulekezi na aidha usaidizi wa kiuchumi hasaa wakati nilipopunguza darahimu wakati wa vipindi vya masomo yangu.

Ninaweza kukosea nikiwasahau wanafunzi wenzangu kama vile, Watuha ambaye kila wakati aliniarifu masuala ibuka, J. Murage, Oluga, Mburu, Mwanjala na pia Amos. Wote hawa tulikuwa abiria kwenye jahazi moja, tulitagusana na kutangamana kwa pamoja.

Ni vyema na haki kuwanyunyizia shukrani zangu kwa wasimamizi wa maktaba za vyuo vya Nairobi, Kenyatta na Laikipia kwa kunipa nafasi  ya kudurusu vitabu, na kuitumie maktaba yao kadri ya uwezo wangu.Narudishia shukrani za dhati kwa msimamizi wangu Dkt.Tom Olali kwa kunitunuku picha halisi za mtunzi na kazi ya usanii aliyoifanya ili utafiti wetu uwe hai.

Ninakerwa moyoni kutaja shukrani zangu zingine kwa walimu wa shule ya msingi ya Siron, Shule ya Dei ya Gatero kwa kunipa mutisha na heri ya kuendeleza na kusanifishia usomi wangu wa kiwango hiki cha uzamili.

Maulana awatunukie Baraka na hekima ili sote tuwe wanja wa kuigwa na kizazi kilioko na cha kesho.

# MUHTASARI

Somo letu la utafiti linashughulikia matumizi ya taswira kama kigezo cha kufanikisha maudhui katika *Utendi* wa *Siiraji.*

Utafiti wetu unanuia kuchunguza kigezo cha taswira na umuhimu wake katika kufanya maudhui ya mtunzi yawe ya kutambuliwa na kuthaminika na msomi .

Kwenye sura ya kwanza tumechunguza masuala; Mwanzo tumetanguliza kuhusu mada tunayoshughulikia, tatizo la utafiti, nadharia tete, umuhimu wa kushughulikia mada , upeo na mipaka, yaliondikwa kuhusu *Utendi* wa *Siiraji,* msingi wa nadharia na njia ya utafiti. Taswira tunayoishughulikia ni taswira chanya inayofungamanishwa na maudhui ya utendi tunaouhakiki.

Sura ya pili inahusu historia ya mwandishi. Sura hii inatoa maisha ya mtunzi, Muhammadi Kijumwa kwenye daraja zifuatazo; asili yake, elimu, ndoa yake, ndoa ya Kiislamu, Ndoa ya Kikristo, asasi halisi ya mtunzi, mchango wake kwenye uwanja wa fasihi, kazi alizozitunga, kazi alizozinakili, kazi alizotafsiri, nyimbo alizotunga, tutumbi na barua alizoandika, uhusiano wake na wageni na pia wenyeji, dini na imani ya mtunzi.

Sura ya tatu imeshughulikia dhana ya talaka kwa mjibu wa dini ya Kikristo, Kiislamu, dhana ya maadili kwenye tungo za kishairi, na dhana ya taswira.

Sura ya nne ndiyo upeo wa utafiti wetu kwani inashughulikia asili ya *Utendi* wa *Siiraji,* dhana ya maudhui kwenye utendi na jinsi kigezo cha taswira kimeunganishwa na maudhui. Maudhui makuu yanayojitokeza kwenye utendi kama vile; ushirikiano, ukarimu, tabia njema, usiri, suluhisho na mapatano, asasi ya ndoa, bidii, wema na utu, usikivu na uelewaji.

Mwisho ni sura ya tano, ambayo inasheheni hitimisho la kazi nzima na mapendekezo kuhusu uhakiki uliyo shughulikiwa. Ni sura hii ambayo imependekeza kazi kadhaa ya utafiti wa ziada.

## YALIYOMO

**UKURASA**

Ungamo ........................................ ii

Tabaruku ........................................ iii

Shukrani ........................................ iv

Muhtasari ........................................ vi

**SURA YA KWANZA** ........................................ 1

1.0 Utangulizi ........................................ 1

1.1 Usuli ........................................ 3

1.2 Tatizo la utafiti ........................................ 6

1.3 Madhumuni ya utafiti ........................................ 7

1.4 Nadharia tete ........................................ 7

1.5 Sababu za kuchagua mada ........................................ 8

1.6 Upeo wa mipaka ........................................ 9

1.7 Msingi na nadharia ........................................ 10

1.8 Yaliyoandikwa kuhusu somo hili ........................................ 16

1.9 Mbinu za utafiti ........................................ 23

**SURA YA PILI** ........................................ 24

2.0 Maisha ya mtunzi kijumwa ........................................ 24

2.1 Utangulizi ........................................ 24

2.1.1 Asili ya mtunzi ........................................ 26

2.1.2 Kuzaliwa ........ 27

2.2 Elimu ya mtunzi ........ 28

2.3 Asasi ya ndoa ........ 29

2.4 Ndoa kwa mujibu wa sheria za serikali ya kenya ........ 30

2.5 Ndoa ya kiislamu ........ 31

2.6 Ndoa ya kikristu ........ 32

2.6.1 Maisha ya ndoa ya mtunzi ........ 33

2.7 Mchango wa kijumwa kwenye uwanja wa fasihi ........ 34

2.8 Kazi zilizotungwa na kijumwa mwenyewe na kuwanakilia kwa hati ya kirumi watalaamu wa kigeni ........ 35

2.9 Kazi zilizotafsiriwa na kijumwa na kuzinakili kutoka hati za kiarabu hadi kwa hati za kirumi ........ 37

2.10 kazi alizozitafsiri kijumwa kutoka kiarabu hadi kiamu na baadaye kuzinukuu . 37

2.11 Nyimbo zilizotungwa na kijumwa ........ 38

2.12 Hadithi ........ 39

2.13 Tutumbi na barua ........ 39

2.14 Kazi alizotafsiri kutoka kwa lahaja moja hadi nyingine ........ 40

2.15 Uhusiano wa mtunzi na wageni na wanajamii ........ 40

2.16 Usanaa wake katika nyanja zingine ........ 41

2.17 Imani na dini ........ 43

2.18 Hitimisho ........ 47

**SURA YA TATU** ........ 48

3.0 Utangulizi ........ 48

3.1 Dhana ya talaka kwa mjibu wa dini ya kiislamu ........ 48

3.2 Misingi ya talaka kwa mujibu wa uislamu .......... 50

3.3 Misingi na sababu ya talaka .......... 51

3.4 Uadilifu kwenye tungo za kitendi .......... 53

3.5 Dhana ya taswira .......... 55

3.6 Hitimisho .......... 59

**SURA YA NNE** .......... 60

4.0 Utangulizi .......... 60

4.1 Asili ya utendi wa siiraji .......... 60

4.2 Dhana ya maudhuI .......... 62

4.3 Maudhui ya *utendi* na taswira husika .......... 62

4.3.2 Umakini .......... 64

4.3.4 Ukarimu .......... 65

4.3.5 Wema na utu .......... 66

4.3.6 Tabia ya wakati wa maankuli .......... 67

4.3.7 Utovu wa nidhamu .......... 68

4.3.8 Suluhisho na mapatano .......... 69

4.3.9 Uasi wa ndoa .......... 70

4.3.10 Utiifu .......... 71

4.4 Mafunzo muhimu .......... 72

4.4.1 Utamaduni .......... 73

4.4.2 Malezi bora ya watoto .......... 73

4.4.3 Uvumilivu na subira .......... 74

4.4.4 Usikivu na uelewaji .......... 74

4.4.5 Imani .......... 75

4.4.6 Kutenda haki na ukweli ........................................................................ 77

4.4.7 Uadilifu ............................................................................................ 78

4.4.8 Hitimisho .......................................................................................... 78

**SURA YA TANO** ..................................................................................... 79

5.0 Hitimisho na mapendekezo...................................................................... 79

5.1 Utangulizi................................................................................................ 79

5.2 Mapendekezo ya utafiti .......................................................................... 81

Marejeleo ...................................................................................................... 82

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Utafiti wetu unanuia kuangazia kama kigezo cha taswira kina umuhimu wowote katika fasihi na hasa wakati mtunzi anapokitumia kwa ueledi na kwa njia ya kiufundi ili kurahisisha uelewaji wa maudhui kwa msomaji au hadhira yake bila ugumu wala kukisia tu. Jee, matumizi mwafaka ya taswira hufanya usanii uwe hai? Haya ndiyo maswali ambayo tunatarajia kuyajibu katika utafiti wetu.

Ni dhahiri kuwa mtunzi hawezi akakaa chini na kuyapanga maudhui anayotaka kuwasilisha, bali maudhui ni matokeo ya uwasilishaji wa sanaa iwe ya riwaya, tamthilia, shairi au fasihi yoyote ile. Mtunzi hana budi kufinyanga lugha ili awasilishe ujumbe wake na taarifa yake kwa kina na kwa njia ya kiufasaha. Endapo msanii hatazingatia matumizi ya taswira, ni kweli kuwa ujumbe utaparaganyika? Au ni kwa kukisia tu? Haya ni baadhi ya maswali yatakayojibiwa na uhakiki wetu kama tulivyokuwa tumetaja hapo awali.Kwa upande mwingine tutadadisi maudhui muhimu yanavyojitokeza kwenye *Utendi* wa *Siiraji* ambayo yananuiwa kuusiwa kijana Helewa na babake .Mtunzi ananuia maudhui haya yawe kama dira na ngao ya kutumiwa maishani mwake.

Kimani Njogu (2008:21), anafafanua maudhui kama ujumbe wa jumla kuhusu matukio, kitu, wahusika, au hali ya maisha kama yanavyojitokeza

Maoni haya yatatufaa katika utafiti wetu kwani maudhui yana maingiliano makubwa na ujumbe unaokusudiwa kuwasilishwa kwa hadhira na mtunzi wa sanaa husika. Ujumbe wa matini katika Utendi kwa kawaida huwa ndio malighafi ya maudhui yaliyowasilishwa na mtunzi kwa njia ya kinathari.

Syambo na Mazrui (1994;46) wanasema ya kwamba, maudhui yanaweza kuwa ya kuonya, kutahadharisha, kuburudisha, kuelimisha, kuipa jamii mwelekeo miongoni mwa mambo mengine.Maoni haya yatatufaa katika utafiti wetu kwani Utendi tutakaouhakiki ni wa kiwaadhi ambao lengo lake ni kuwausia wana na walezi na kuwaekeza katika misingi ya hulka na tabia njema ,ili iwe kama kielelezo cha maisha yaliyofunganyika na maadili mwafaka ambayo yana paswa kuigwa na binadamu yeyote. Mtunzi wa *Utendi* wa *Siiraji* alinuia kumuusia mwanawe Helewa wasia huu kama tuzo na urithi wa kumfaa aushini mwake.Aidha alitarajia utenzi wenyewe uhifadhiwe kutoka kizazi kimoja hadi kingine ili kuwafaa kwa kutumia nyaadhi kama hii ya maadili mwafaka kama itakavyofafanuliwa zaidi kwenye utafiti wetu.

Ni wazi kusema kuwa mwandishi hupandwa na jazba na kukata ushauri wa kuwasilisha ujumbe fulani kwa njia ya kiubunifu na kuandikia wanajamii wake ili wafaidike na ujumbe ulioko kwenye usanii wake. Kulingana na wanasanii wengi wa kimagharibi ni ya kwamba mhakiki huwa na fahamu ya jamii yake kiasi cha kuadhiriwa na jamii yake na kuandika yale yanayoipa jamii mwongozo mzuri wa kimaisha. Tolstoy (1948) anaitazama fasihi kama zao la jamii na kuwa fasihi itaeleweka tu inapohusishwa na mazingira ya jamii inayoizalisha. Kwa maoni yetu tunaamini mada hii na mtafiti yeyote tunayemfahamu.Uhakiki wetu unanuia kuchunguza namna mtunzi waUtendi wa Siiraji Mohammed Kijumwa amefaulu kuwasilisha maudhui yake kwa kutumia kigezo cha taswira kama mbinu mojawapo ya utunzi wake.

Lengo letu ni kutadhmini ni kwa kiwango kipi, amefaulu katika jitihada zake za kuusia mwanawe Helewa, wasia wake ambao anauita *Siiraji* **(Taa)** kwa kutumia mbinu ya taswira.

Tunatarajia kwamba tumeuzimba mwanya huu kiutafiti na kufaidika na uhondo wa utendi hasa kazi hizi za kimapisi.

## 1.1 USULI

Ushairi andishi wa lugha ya Kiswahili una historia ndefu tangu fasihi simulizi ya Kiswahili ilipoanza kuandikwa kwa hati ya Kiarabu tangu karne ya 11. Mlokozi (1999) anasema tenzi ni tungo ndefu za ubunifu ambazo maudhui yake yanajikita katika masuala ya kidini, mbeko, utamaduni, na historia .Aidha

Mnyampala (1965) anasema kuwa Waswahili walikuwa wakifungiana nyama kwa kubuni tendi na mashairi ili kuwasilisha mawazo yao. Mashairi na tendi nyingi kabla ya majilio ya wageni hasa katika upwa wa Afrika Mashariki, yalikuwa yanatungwa na kuimbwa kwenye ngoma za jando, unyagoni, na tumbuizo za sherehe za jamii nyingi za Kiafrika.

Majilio ya Waarabu katika eneo la Afrika mashariki yalileta dini ya Kiislamu na athari yake, tamaduni na mbeko za Uarabuni. Athari hizi zilipenya katika nyanja zote za maisha kama vile kielimu, kiuchumu, kiutawala, kiutamadani, kisiasa na hata kidini. Baadhi ya Waafrika waliweza kusilimu na kuteuliwa kuwa viongozi na maimamu wa dini ya Kiislamu. Kwa upande mwingine Waarabu waliibua usanii wa kuandika kwa hati za Kiarabu na kwa mara ya kwanza, fasihi simulizi ya Kiswahili ikaanza kufasiriwa kwa hati ya Kiarabu. Ukoloni na utawala wa Wareno uliofuata utawala wa Waarabu wa Omani mwishoni mwa karne ya 18, pia ulinufaisha fasihi simulizi kwa kutumia na kuhifadhi fasihi hiyo kwa hati za Kireno na hasa katika upwa wa Afrika Mashariki.

Allen (1938)anadai kuwa baada ya majilio ya ukoloni katika upwa wa Afrika masharikі na fasihi simulizi kuandikwa kwa lugha za kigeni,tendi zilianza kufasiriwa na kuandikwa kwa hati ya Kirumi .Kwa mfano *Utendi wa Fumo Liyongo* uliotungwa na kutafsiriwa na mtunzi Muhammadi Kijumwa ni miongoni mwa Tendi za zamani zilizotafsiriwa kwa lahaja za kiswahili kwa umaarufu wake.

Athari ya dini ya Kiislamu ilipenya zaidi katika uandishi wa fasihi ya Waswahili hivi kwamba watafiti wengi wa fasihi hii walidai kuwa endapo utendi haungetangulizwa na fomula maalum kama vile sifa za Mungu, Mtume Muhammadi na aila yake sifa ya masufi na wafuasi wa dini ,basi huenda kuna baadhi ya beti ambazo zimeondolewa.

Steere, (1970:39) anasema kuwa tendi nyingi ziliangazia maudhui ya dini ya Kiislamu kwani wengi wa waandishi walikuwa wamesilimu na kuwa wafuasi shupavu wa dini hiyo na hivyo kuathiri na maudhui ya kidini.

Knappert (1967:49) anadai fomula hii ya utunzi ilizingatiwa na takribani wote wa tendi za zamani kama inavyodhihirika katika utangulizi *Utenzi wa Miiraji* ambao unasema;

*Bisimillahi, arahamani rahimu*

*Nanza kunudhumu kwa isiimu yake*

*karima mola Mu'adhamu mtukufu*

*mwenye rehema……. Ub1*

Mtunzi amepenyeza fomula hiyo kwa kiueledi. Walakini sifa za Mungu na umuhimu wa imani ya Kiislamu umesheheni beti nyingi kama ilivyokuwa kaida ya tungo njingi za kiutendi. Katika ubeti wa 5 mtunzi ametoa sifa za Maulana na kufaulu kukwepa ukiushi wa mtindo wa fomula hii ya Tendi.

*Kwanda baba mcha Mungu*

*Utaokoka mwanangu*

*Huku huko kwa utungu*

*Ukosa cha kutumi. Ub.5*

Waswahili kwa upande mwingine walitilia maanani waadhi kama desturi na uridhi kwa wanao na kila mlezi aliwajibika kuwausia wanawe kabla hajaenda zake. Wasanii gwinji kama vile Muhamadi Kijumwa,Mwanakupona binti Mshamu walibuni tungo za kiwasia za kuigwa na wanajamii ili kuyapa maisha yao thamani sio tu kwa kizazi kilichokuwapo bali hata kwa nasaba iliyofuata baadaye. Kwa mfano nyimbo, ng'ano na Tendi zilitumiwa kama vifaa vya kuwasiliana na kujuliana hali miongoni mwa wanajamii na taa ya kumulika mienendo na tabia zao za kila siku.

Uhakiki wetu umepata misikumo kutokana na falsafa pevu ya kimaisha iliyojikita na kuwasilishwa na mtunzi katika *Utendi* wa *Siiraji.* Neno "Siiraji''maana yake ni "taa" na chuo cha Siiraji maana yake ikiwa "Kitabu cha taa".Mtunzi katika utungo wake anawazia kifaa hiki kuwa kama mwongozo bora zaidi wa kuigwa na mwanawe aidha walimwengu kwa jumla. Utungo wote umetumiwa kuonyesha motifu ya maisha yenye uadilifu ambayo anapaswa kuigwa na kizazi chochote chenye ari ya kutenda wema.Ni wazi kutaja kuwa Nuru au mwangaza hufananishwa na Allah , sio tu kwa kitabu kitakatifu cha *Qu'ran* bali hata *Biblia*; Malaki; (4;21)Yesu amesema kuwa taa haifichwi chini kitanda bali huwekwa pahali wazi panapofaa kila mtu. .Mfano mzuri ni katika sura ya *Qu'ran* tukufu Sura ya 24:35 ambayo inasema "***Mungu ni mwanga wa mbingu na arthi.***" Ni katika Ubeti 4 ambao dhana hii ya mwangaza inadhihirika zaidi kama kifaa huku kifaa kitoacho miale ya mwanga kwa wale wanaokitumia;

*Chuo hiki ina lake*

*Ni Siraji uishike*

*Kwa wanaume na*

*Wake wape wakitembelea . Ub 4*

Knappert (1967;87) anasema kuwa Mtume Mohammed anafananishwa na nuru ambayo Mungu aliiumba kwanza.Ndiposa Mtunzi alibuni dhana hii ya taa kama anwani ya utenzi wake na iwe kama mwangaza wa kumwongoza mwanawe Helewa katika maisha ya ulimwengu uliojaa maovu na majaribio mengi.

## 1.2 TATIZO LA UTAFITI

Mtunzi wa Utendi wa Siiraji ametumia taswira kama mbinu kuu ya kuwasilisha ujumbe wake.

Tunataka kutathmini, kufaulu au kutofaulu kwake katika kuwasilisha ujumbe kwa hadhira lengwa.Je, matumizi ya taswira yana mvuto wowote kwa msomaji wa *Utendi wa Siiraji*?

Je mwandishi amefanikiwa kutumia taswira ya aina gani kuwasilisha maudhui yake.Kama tunavyoelewa taswira inaweza kuwa kuwa hasi au chanya. Je, mwandishi mwandishi wa utenzi huu amezingatia taswira ipi zaidi katika kufanikisha kazi yake? Je, taswira hizi mbili zimetumiwaje kuyaangazia ambayo mtunzi anataka kuyakweza nayale ambayo anataka kuyadunisha au kuyadhalilisha.

Haya ni baadhi ya maswali ambayo yanatupa hamu ya kuitafiti utendi huu wa Siiraji ili kuangazia mafanikio ya mbinu ya taswira katika kufanikisha lengo la mtunzi Muhammad Kijumwa.

Ni bayana kusema kuwa kila msanii hutamani kazi yake ya kiusanii iwe ya kipekee na ya manufaa kwa hadhira aliyolenga ili iwe johari kwa kuwahekimisha na kuwafaidi kwa njia moja au jingine.Vivyo hivyo utafiti wetu umenuia kuzimba pengo la kiutafiti kadiri ya ufahamu wetu.Utafiti huu umechunguza

Matumizi ya taswira kama kigezo cha kufanikisha maudhui katika utendi wa Siiraji, uliootungwa na Muhammadi Kijumwa.

## 1.3 MADHUMUNI YA UTAFITI

Malengo yetu katika utafiti wetu ni kudadisi jinsi mtunzi wa *Utendi* wa *Siiraji* anavyofanikiwa kutumia kipengele cha taswira ili kuvuta hisia za msomaji na kufanikisha uelewaji wa ujumbe ulionuiwa.

Aidha utafiti huu unanuia kubaini na kuangaza jinsi kipengele cha taswira kilivyotumika ili maudhui yaeleweke kwa uwazi zaidi bila kuyakisia tu.

Tuna na azimio na ari ya kujaribia nadharia tuliyoichagua ya maadili kama inajitosheleza kuhakiki kazi yetu.Aidha ni matarajio yetu kuwa utafiti huu utasahilisha uelewaji wa *Utendi wa Siiraji* amabao utawapa watu wengi hamu na ari ya kuusoma na hivyo kuyasambaza mawaidha yake kwao.

## 1.4 NADHARIA TETE

Ni haipothesia yetu kwamba;

Mtunzi wa *Utendi wa Siiraji* amefanikiwa kutumia mbinu ya taswira katika kuyafikisha malengo yake.

Mbinu ya taswira imefanikiwa kuziteka hisia za msomaji wa *Utendi wa Siiraji.*

Mbinu ya taswira chanya imetumiwa zaidi katika kuendeleza maudhui ya mtunzi wa *Utendi wa Siiraji*.

Nadharia ya maadili inajitosheleza katika kuuhakiki *Utendi wa Siiraji.*

## 1.5 SABABU ZA KUCHAGUA MADA

Kila mhakiki ana sababu na misukumo inayomshawishi ili achague mada fulani ya utafiti wake. Tumehiari kuchagua mada hii ya matumizi ya taswira katika *utendi wa Siiraji* kwa sababu kadha wa kadha .Kwanza kwa maoni yetu hakuna ithibati yoyote ya kuonyesha mada hii imewahi kuhakikiwa na mtafiti yeyote huku kipengee cha taswira kikitumiwa kama kigezo cha mada yake. Aidha, utafiti huu utakuwa wa manufaa kwa wasomi na watafiti watakaopata nafasi ya kudurusu kazi yetu.

Wahakiki wengi wametumia kipengele hiki cha taswira kuhakiki kazi zingine za kifasihi walakini hawajahi kufanyia utafiti *Utendi* wa *Siiraji.* kwa mfano; Momanyi (1998), ametumia kigezo cha taswira kuhakiki *Utendi wa Al-Inkishafi.*

Mogere (2007) ametafiti kwa mada hii ya taswira kwa kuonyesha picha kamili ya gereza inavyoendeleza maudhui katika riwaya ya *Haini.* Ni baada ya kuyatafakari hayo na kutaka kutoa metonumia ya tendi kwani zimepuuzwa na wengi.

Topaz (1971:6) anasema kuwa tafiti nyingi kwa maoni yetu zimeshughulikia maswala ya kiwakati kama vile ufeministi na kupuuza sanaa za maadili kwani na haoni hulka za watoto wetu zinazorota kwa kukosa wa kimaadili.

Jitihada zetu za uhakiki wa *Utendi* huu itakuwa hatua kubwa na yatamanika ili maudhui yatayojitokeza yaweze kuigwa na wengi kwa manufaa yao ya kimaisha. Aidha Wahakiki wengi wameshughulikia mashairi na fasihi ya kileo na kupuuza

tahakiki za kijadi zenye uasilia na utajiri mwingi sana wa falsafa ya maisha kama vile tendi na ng'ano za awali.

Katika kuibua tahakiki hii tunatarajia tutakuwa kupiga hatua ya mbele kwa utafiti wa tendi za kijadi na kuwa miongoni mwa wahakiki wa kazi za kimapisi.

Kilichotupa moyo na jazba ya kuhakiki *Utendi* huu ni kuwa mtunzi ni gwiji katika uwanja wa sanaa. Tunaonelea kwamba kuchambua kazi mojawapo yake ni njia moja ya kumbukizi za usanaa wake. Kwa kuangazia historia ya Muhammadi Kijumwa, tutakuwa tumetanda sifa mahsusi zinazostahili kupewa mwanafasihi kama huyu aliyesheheni na kupewa sifa mwafaka na wageni na wanajamii wake.

Utendi huu una maudhui yenye falsafa ya kimaisha ambayo mafunzo yake anawafaa wanajamii wote duniani kama itakavyojitokeza. Maudhui ya utendi huu hayaegemea upande wa dini ya kiislamu kinyume na Tendi nyingi, bali tendi hili limeangazia uhalisia wa maisha kama vile; ndoa, tabia, utu mambo ambayo ni ya kimsingi katika jamii zote ulimwenguni. Ni katika utambuzi huu ambao utafiti wetu unapata msukumo na sababu murua ya kuhakiki mada hii.

## 1.6 UPEO WA MIPAKA

Uhakiki huu ni wa kifasihi .Tunakusudia kuangazia matumizi ya taswira katika kuendeleza malengo ya mtunzi wa *Utendi wa Siiraji.*

Utafiti huu umejishughulisha nasuala la maudhui na hasa yanayoangaziwa na mbinu ya taswira. Suala la fani limerejelewa tuiwapo litakuwa likichangia utafiti wetu.

Utafiti wetu ni wa maktabani tumetajia kunufaika kutokana na tafiti nyingi ambazo zimeangazia suala la taswira.

Aidha tutawahoji wanafasihi wengi na hasa wanaoshughulikia tendi ili kunufaika na mawaidha yao.

Tumetarajia kupata msaada msaada mkubwa katika mtandao ili kufanikisha utafiti huu.

## 1.7 MSINGI NA NADHARIA

Katika utafiti huu, tumeongozwa na nadharia ya maadili. Mwasisi wa nadharia hii ni mwanafalsafa wa kiyunani wa enzi ya urasimi anayeitwa Plato (?). Plato ndiye amehusishwa na mtazamo huu wa maadili na maoni yake yameangaziwa kwenye vitabu vyake; *The Republic,Ion* na *The Law*.

Wamitila (2003:266) anasema kuwa mwasisi huyu ameshikilia imani ya kwamba, mashairi sharti yangechunguzwa ili kuchuja athari chanya ambazo zingeweza kuigwa na jamii na hasa vijana. Aidha mwasisi huyu anachukua dhana ya mwigo katika ushairi, maana ya ushairi na kuieleza kuwa na dosari

Maoni yake Plato ilikuwa mshairi ni mwigaji tu asiye na maarifa yoyote.juu ya hali halisi anayoiigiza yeye mwenyewe.

Kimani (2008:10) anasema kuwa msanii huwakilisha jamii.Maoni yanayojitokeza si ya msanii bali ni ya jamii pana.

Mwasisi huyu ameshikilia kuwa ushairi lazima utumikie mtu, umnawirishe kiroho na kumpa uadilifu wa jamii. Dhima imeangaziwa zaidi hata kwa wahakiki wa baadaye ambao wanasisitiza dhima ya fasihi na jamii kwa ujumla.

Plato anadai kuwa endapo kizazi kijacho kingewajibiwa kwa uongozi wa nchi, basi inafaa kizazi hicho kisihusishwe na sanaa hasi yenye miigo ya watu wenye hulka hasi au waigizaji ambao wamepotoka kimaadili. Sanaa kama hiyo aliiona yenye athari potovu kwa watoto wachanga wanaojifunza lugha, tabia na huenda wangeiga mwigo usiokubalika na desturi za jamii nzima. Mwanafalsafa huyu alihofia kuwa endapo hadhira ingeiga sanaa hiyo ingekuwa changamoto kwa jamii na utawala wan chi kwa ujumla.

Kwa upande mwingine alisisitiza kwamba usanii wowote sharti uhakikiwa na Jopo la wataalamu wanao ueledi wa fasihi na wayapishe au kuzipuuze fasihi ambazo wangeziona ni hasi kwa jamii na kwa hadhira kwa ujumla ila nadharia ina jukumu na utendakazi wake katika kawazi inayokusudiwa. Kwa mikabala ya utafiti wa kifasihi ushirikishi wa nadharia huwa ni chanzo cha kumwelekeza mtafiti kwa misingi na mihimili ya nadharia hiyo. Kila nadharia hufaa kwa kuhakiki utafiti fulani kuliko nyingine hasaa kulingana na tatizo lenyewe.

Uhakiki wetu ni wa Utendi wa ki*wasia.* Utendi wa kiwasia hujihimili kwenye mihimili ya kimaadili huku misingi yake ikiwa kuimarisha na kudumisha maadili mema ya kibinafsi na jamii kwa ujumla. Nadharia ambayo imetufaa katika utafiti wetu ni nadharia ya Maadili. Kunao wahakiki wengi wanaohusishwa na nadharia hii. Wamitila (2003) anadai kuwa dhana ya maadili hutumiwa kuelezea usomaji na tathmini ya kazi za kifasihi kwa kuangalia uhusiano wake na ubinadamu na hasa maswala ya kimaadili badala ya kuzingatia ujumi wa kazi hiyo. Nadharia ya maadili mwanzo ni vyema kutaja waasisi wa nadharia hii ya kiuadilifu.

Kulingana na kamusi ya Tuki (2008) Uadilifu ni "hali ya kutenda bila ya kupendelea upande wowote" Uadilifu kwa maoni yetu ni hali ya kutenda mema bila kushurutishwa na mtu yeyote. Maadili hayawezi ikatenganishwa na mbeko za jamii kwani wanajamii ambao hawazingatii maadili mema katika desturi na mbeko zao huwa ni jamii iliyotupa mwelekeo ulimwenguni.

Sherman (1971:51-63) anasema kuwa mbeko ni sheria ambazo huhifadhiwa na utamaduni wa jamii ambazo huthaminiwa na kuridhiwa na kizazi kimoja hadi kingine. Maoni haya ya mhakiki huyu yanaafikiana kuafikiana na yetu kwani mbeko ndizo sheria zinazofuatwa na wanajamii huku zikijikita kwenye tamaduni zao na kuwa na maadili mema ya kutamanika na kila mwalimwengu.

Njogu (2007:24) anasema kuwa maoni ya Plato kwa upande mmoja yana manufaa na ilhali upande mwingine yanawezakuwa kuwa magumu kuyatekeleza madai na sheria kama hizo kwa wakati huu. Tukichukulia enzi za kisasa itakuwa ni vigumu sana kuhakikisha uandishi wote ambao unasomwa na kuwafikia wanajamii umepitia kwenye mizani na sheria za utawala kwani nchi nyingi ni za kidemkrasia na zenye kulinda haki za kila mwananchi.

Teknolojia imebuni njia mbalimbali za mawasiliano na ingali inatafitiwa ili kupata mawasiliano rahisi na ya kisiri zaidi.Wanajamii wamepewa uhuru na demokrasia ya kutumia vifaa vya mawasiliano bila vizingiti vigumu ya kupitisha ujumbe wao.Mitambo kama vile tarakilishi imeivumbuliwa ili kurahisisha kazi ya mawasiliano. Walakini kila tapo lina uzuri na upungufu wake. Kwa mfano kwenye mtandao wa simu na tarakilishi unaoitwa '*surakitabu.*'

Mtandao huu umetumiwa kwa njia mbaya na kudunisha hulka na maadili ya wanajamii hasa vijana wanapowasiliana. Wanafalsafa wa enzi hizo za Kiurasimi wangekubali mitandao kama hii iliyo na uhuru mwingi usiochunjwa na sheria za nchi?

Kulingana na maoni ya Plato watoto na vijana wanastahili kukua na tabia ya kutii sheria za nchi yao na wala sio kinyume chake na jukumu la msanii ni kumwelekeza msomaji jinsi ya kuwa mwanajamii bora.Waasisi wa nadharia hii ya maadili wanasema fasihi kuwa ina majukumu ya kuyafichua maovu yaliyopo katika jamii na kuelekeza jamii kwenye mema kwa kubainisha njia ya kuushinda uovu.

Senkoro (1988) akilichanganua wazo la Plato anadai msisitizo kuhusu dhima ya uelimishaji inayojitokeza katika ushairi na ambao kwa hakika ulienea kote Ugiriki wa zamani ule ulijitokeza mno katika maandiko ya Plato, ushairi ni lazima utumikie mtu kiroho, umnawirishe kiroho na kumpa uadilifu wa kijamii.

Mawazo ya Senkoro kumhusu Plato ni ya kiwakati, kwani fasihi inastahili kuhekimisha jamii, kuangazia uhalisia wa jamii na fasihi kuwa chombo cha kuelekeza na kushauri jamii kuiga na kudumisha maadili mema kwa manufaa yao na ya jamii zingine.

Kwa kiwango kikubwa tunakubaliana naye kwani fasihi ni malighafi ya jamii na kifaa cha kuadili jamii. Walakini hatukubaliani naye wakati anapohimiza kuwa fasihi iwe na wadhifa wa kuwasifu viongozi na utawala na wala sio fasihi isitumiwe kuwakashifu. Tunajua ya kwamba fasihi ina uwezo wa kuunda jamii yenye maadili mema kwani viongozi wanastahili kuwa kielelezo kwa jamii nzima ili iwaige kwa

mienendo yao dhabiti. Fasihi inastahili kuyafichua, na kuyamulika maovu ya viongozi na wanajamii kwa ujumla ili wawajibike.

Ginn (1960:66) anasema kuwa Aristotle (384-322KYM) ni mwanafalsafa mwingine wa Ugiriki ambaye alikuwa mwanafunzi wa Plato ameungama na maoni yake juu ya nadharia ya maadili. Amekuwa na maoni yaliyokaribiana na Plato kuhusu falsafa ya maisha, siasa, na utawalhasa.Kuhusu uwakilishi wa mwigo Aristotle amesema kuwa mtu mtu hufurahia zaidi mwigo wa uhalisi wenyewe ,hasa pale hisia kama zile za hasira ama woga zinahusika .Alidai kuwa watu hupenda kuona ,kwa mfano samba akiwa amewakilishwa katika sanaa kuliko kumwona samba mwenyewe.

Kwa maono yetu ushairi wa awali wa Kiswahili umehusishwa sana na jamii.Zaidi umelenga katika kuiadilisha jamii kupitia maudhui ya sanaa.

Wamitila (2003) anadai kuwa Aristotle ambaye alikuwa mwanafunzi sugu wa Plato alikuwa mtetezi wa dhana ya mwigo. Aliamini kuwa sanaa ni mwigo au uigaji wa maisha ya binadamu.Fasihi kwa mtazamo wao inakuwa kielelezocha jamii.

Mwanafalsafa huyu aliamini kuwa sanaa ilikuwa ufananisho halisi wa jamii na hivyo basi kuna uwezekano wa vijana kuiga walichokiona kwani maisha kulingana na mwanafalsafa huyu ni mwigo wa yale tunayoyaona. Kulingana na mwanafalsafa huyu, Mwigo una malengo ambayo unastahili kutekeleza kwenye maisha.

Dhana moja kuu ambayo waliitazamia kuwa msingi wa madai yake ni kuwa binadamu ameubwa akiwa kiumbe kisichokamilika na kinahitaji kurekebishwa kwa njia ya usanii.

Tolstoy (1948) anadai kuwa sanaa inastahili kufunza zaidi kuhusu huduma ya jamii, Utu, huruma na upaji na wanajamii kuepukana na uhoro, tamaa na tabia zote zinazokiuka mbeko za jamii hiyo.

Tolstoy anaamini ya kwamba sanaa huleta ushirikiano miongoni mwa watu, na utangamano wa jamii zote ulimwenguni Kwa ujumla wake.

Mawazo ya Tolstoy yatatufaa katika uhakiki wetu kwani kwani utendi tunaouhakiki ni wa kimaadili na msingi wa Tendi za kiwasia ni kukejeli maovu ya mtu na jamii kwa ujumla. Tolstoy aliamini jamii ambazo hazijagawika kwa misingi ya kitabaka na zenye kumcha Mungu na uwezo wake kwa waja wake. Kulingana na mhakiki huyu aliamini kuwa misingi ya dini ni ishara timilifu ya kuadili mwanadamu na kukiuka na maovu.

Msokile (1993:6) anasema kuwa nadharia ya maadili inahimiza kuwa nguzo ya nadharia hii ni kuwa umuhimu wa fasihi hautokani tu na jinsi ya kusema bali ni kwenye kile kinachosemwa (kiashiriwa). Mara nyingi hii huelezwa katika mtazamo wa "fani na maudhui". Tofauti na mkabala wa kiufafanuzi ambao husisitiza ama kujali jinsi ya kusema jambo. Maoni ya mhakiki huyu yana ujumbe sambamba na wanafalsafa wa Kigiriki kwani matendo ya uigaji ndicho chanzo cha tabia hasi au chanya itakayopata mashiko katika jamii nzima.

John Hospers (1978) katika jarida lake la *Art and Morality* huku akinukuu kazi ya *Monroe Aesthetics*, anafasili kuwa sanaa ni ukamilisho kwani hutupatia tunachokihitaji na tusichokitarajia kwani ina utoshelevu wake. Maoni ya Hosper ni ya kiwakati kwani kila sanaa ina azimio inayonuiwa itekeleze.

Misingi na mihimili ya nadharia hii kwa muhtasari ni;

i. Mwandishi hulenga kuandika yale yanayojenga jamii kimaadili kwa kuchunja athari mbaya za kazi anayoandikia.
ii. Fasihi hutumiwa kama kielelezo cha jamii kwa kufichua maovu yaliopo katika jamii na kuielekeza na kuipendekeza mema.

Wafuasi wa nadharia hii wanaamini kuwa fasihi ina wajibu wa kuyafichua maovu yaliyopo katika jamii na kuielekeza jamii kwenye mema kwa kubaini njia za kuushida uovu.

Mihimili ya nadharia hii imetufaa kuhakiki mada yetu kwani inapelekana na shabaha yetu ya utafiti .

## 1.8 YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO HILI

Ingawa hakuna ithibati inayoonyesha kuwa somo letu la utafiti limehakikiwa dai hilo haliwezi likawa kizingizio cha kutogusia baadhi ya kazi zingine zinazokaribiana na Tendi za kinyaadhi kama usanii wa kimapisi. *Utendi wa Siiraji* tunaouhakiki umejizatiti misingi ya *kiwasia.*

Knappert (1967:13) anadai kuwa dhana ya wasia, usia au waadhi ina ujumbe ambao unalenga kuboresha hulka ya muusiwa ili mienendo yake ili shwari sio tu kwake yeye mwenyewe bali iwe ni kioo cha kuigwa na jamii nzima.

Wahakiki wengi wa kigeni hawakutatathmini na kupata tofauti kati ya utamaduni wa Waswahili Waislamu na itikadi ya dini ya Kiislamu iliyoenea eneo la Afrika Mashariki. Trimingham (1964) anaunga mkono wazo hili kwa kunena kuwa,"mtu aliyesilimu alibaki kuwa Mwafrika hata kama ilimbidi afuate mbeko za uislamu kama vile "faradhi" na "Sunna".

Mienendo kama hii ya kidini haikuasi mila na desturi ya Kiafrika kwani ilijidhirisha katika kazi yao usanii wa kimaandishi hasa nyimbo za jandoni, unyagoni, mashairi, tendi na hadithi za kiushauri. Hapa tunataka kuangazia ya kwamba waswahili kama waafrika wengine walitumia mbinu za aina mbalimbali kuilekeza jamii zao ili ziwe adilifu.

Waswahili walitumia Tendi za kiwaadhi kupenyeza misimamo, mapendekezo, na jinsi wangetaraji hulka za watoto wao ziwe.Yafaa tujikumbushe kuwa hata watunzi ni wazazi na wana jukumu la kulea watoto wao na kuigwa kama vielelezo vizuri miongoni mwa jamii.

Tendi ambazo ni za kiwaadhi na kusheheni kaida za kiuutendi na ambazo zimekaribiana na utendi tunaouhakiki ni kama vile; *Utendi wa Mwana kupona, kiokozi cha Banati*, *Waadhi wa ushairi*, *utendi* wa *hati na Utendi wa Adili na nduguze* uliotungwa na Shaaban Robert.Tukiutazama *Utendi wa Mwanakupona* ulitungwa na Mwanakupona binti Mshamu aliyeishi eneo la ziwa Pate upwaa wa Afrika mashariki, una sifa nyingi.Mtunzi anamuusia bintiye Mwanakupona.

Kwenye utangulizi wa Utungowa huu mtunzi ametanguliza utungo wake kwa kumwalika bintiye kwa mashauri, sawia na utangulizi wa *Utendi wa Siiraji* kwa kusema kuwa;

***Nigema wangu binti***

***Mchachefu wa sanati***

***Upulike wasiati***

***Asa ukazingatia*** Ub.1

Kwenye *Utendi* wa *Siiraji* mtunzi anatanguliza kwa kumkaribisha muusiwa wa kiume kwa kusema;

***Keti hapa sikuliwe***

***Mimi sina illa wewe***

***Likupatao uyuwe***

***Babangu alinambia. Ub.1***

Kinge'i (2000) anawazia kuwa *Utendi wa Mwanakupona* ni miongoni mwa tenzi zenye maaadili kwa vijana hasa kwa wasichana wanaojitayarisha kuolewa. Mtunzi huyu ni kielelezo cha mama wa kinyumbani wa karne ya 19 na aliyetia fora miongoni mwa utamaduni na mila ya Waswahili. Utendi tunalouhakiki una ushauri wa pande zote mbili za kike na za kiume.

*Utendi wa Hati* nao ni miongoni mwa tendi za kiwaadhi ambazo ulidhamilia kuusiwa bintiye mtunzi. *Utendi wa Hati* umetungwa na kuandikwa na Shaaban Robert.

Utendi huu ni wa kisasa kuandikwa kwa lahaja ya kiunguja.

Mtunzi ametanguliza kwa kumshauri bintiye ajiandae kwa ushauri na uelekezi wa babake mlezi. Kama inavyojitokeza katika ubeti wa 1 unaosema;

***Leo nataka binti***

***Ukae juu ya kiti***

***Ili uandike hati***

***Ndogo za wasia Ub.1***

Mtunzi anasisitiza tabia, na maadili mema na hasa yanayolenga asasi ya ndoa na maisha kwa ujumla.

*Utendi wa kiokozi cha Banati* umeandikwa na Sheikh Mohammedi Jambeini.. Utenzi huu ulikusudiwa kutoa wasia kwa binti ambaye anatarajiwa kuwa kielekezo cha mabinti wengine wa Kiislamu wenye maadili mema yanayolingana na mafunzo ya dini ya Kiislamu. Katika Ubeti wa 7 na 8, mtunzi ameamua kuwashauri mabanati kutilia masomo na ulezi wa watoto maanani.

Ingawa utendi huu unatilia maanani masuala ya faradhi ya dini ya Kiislamu na kusifu nguzo tano za kiuislamu, bado ni wa kiwasia kwani misingi yake inaafikiana na falsafa ya kimaisha.

Kwenye ubeti wa 7 mtunzi ana ushauri wa kutilia maanani elimu, kwa kuwapa watoto elimu bora. Mtunzi huyu anatilia mkazo masomo na kukiuka desturi uhimizaji wa dini pekee.Mtunzi anasema;.

*Zijina zungu, muyuwe, maana muyatambuwe*

*Shariya mulitatuwe, ibadani kutumiya Ub.15*

*Utendi wa Adili* ambao umetungwa na Shaaban Robert na kuhifadhiwa kwenye *diwani* ya *Pambo la lugha* (1944:43). *Utendi* huu una uhusiano wa karibu na utendi tunaouhakiki. Ni dhahiri kusema kwamba maingiliano ya karibu miongoni mwa tendi za kiwaadhi ni dini.Kwa maoni yetu msisitizo mkubwa sana unatiliwa kwenye kuchukua kwa uzito imani ya dini *ya kiislamu* na uhusiano wa mtu na Muumba wake.

Dhana ya imani imezuka kwingi kwenye tendi za aina hizi za *tendi* za kiwaadhi. *Utendi* wa *Hati* unasisitizia manufaa ya kumtii Mungu, kama inavyojitokeza kwenye tendi nyingi za Waswahili Utendi wa Hati ambao ulitungwa na mtunzi Shaaban Robert kwenye ubeti wa 10 mtunzi anamshauri mwanawe kwa kusema;

***Kwanza mche Mungu***

***Mwengeza ulimwengu***

***Juu akaweka mbingu***

***Nyota zituangazie*** *(Ub.10)*

Maudhui ya kijumla ambayo yanajitokeza kwenye tendi hizi za kiwaadhi ni msisitizo mwingi wa tabia chanya, kuwa na utu, utiifu na kuwa na maadili mema yanayoweza kuigwa na wengine wa karibu. Utiifu wa mke au mme, kufuata maagizo ya dini, na kudumisha asasi ya ndoa yenye furaha ni miongoni mwa maudhui yanayojitokeza kwenye tendi nyingi za kiwaadhi kulingana na utafiti wetu. Kwenye *Utendi wa Hati* katika Ubeti wa 59 mtunzi anamshauri bintiye kuhusu ndoa ya kufanikiwa kwa kusema;

***Sita ukioa mke***

***Kwa mapenzi mshike***

***Simfanyie makeke***

***Ila akuanze yeye. (Ub.59)***

Katika *Utendi* wa *Siiraji* (Ub 171) unaungama na ubeti huu wa *utendi* wa *Hati* wakati mtunzi anapomshauri mwanawe wa kiume kuhusu ndoa kwa kusema;

***Mke wako mpumbaze***

***Kwa uwezalo mweneze***

***Na wewe simetetze***

***Nde ukalimatia (Ub 171)***

Ushauri tunaoupata kwa beti hizo mbili unaweza kuwa wa kudhibitiwa na mme au mke wa jamii yoyote anayetaka dhima na jukumu la kudumisha asasi ya ndoa.

Mnyampala (1965:5) anadai kuwa *waadhi* ulitolewa kwa njia ya ushauri ili kuyasheheni mambo magumu ya duniani, yaliomo miongoni mwa watu wa kila hirimu, "Vijana wa rika moja", kila kabila, taifa na kila dini.Mtunzi huyu katika shairi lake liitwalo *Kifo cha Bwana Robert,* anatumia taswira ambazo zinajitokeza kwenye lugha inayohusiana na mawazo yake.Ub.wa 2 usimulia jinsi kifo cha Shaaban Robert kitakachokuwa pigo kubwa katika ulimwengu wa Kiswahili. Kulingana na mtunzi kifo chake kingefanya Kiswahili kiiname kama vile Jani la mmea uliokosa maji.

*Ni hasara kwa nchi nzima, ninayosema kwa dhati,*

*Ni kama taa kuzima, usiku wa katikati*

*Kiswahili tainama, kwa kukosa kalafati,*

*Kifo cha Bwana Robert, hasara kwa Kiswahili. Ub.2*

Senkoro (1984) anadai kuwa mbinu hii ya taswira humwezesha mpokeaji kupata picha kamili la tukio linajengwa na mtunzi.

Mulokozi (1975), katika utungo wake wa shairi liitwalo *Maisha Yako* linaonyesha taswira ya maisha ya mtu mnyonge wa tabaka la chini.Mtunzi anatanguliza ubeti wa 1 kwanza kwa kuonyesha picha ya ufukara ambayo inajengwa katika maelezo ya makazi ya mtu mnyonge na familia yake;

*Ugali mchungu na kauzu wenye mchanga wamekwisha chunguni,*

*Watoto wanane wamezagaa sakafuni juu ya mkeka unao wazidi umri,*

*Moshi wa kibatari ni mwingi kuliko mwaga wake,*

*Kitanda cha miyaa kinachoalika pempeni,*

*Mbu waliovimba matumbo wanazuzuma ndani ya moshi*...Ub.1

Clara (1998) anasema kuwa taswira ni mbinu kuu ambayo hutumiwa na watunzi wengi ili kuzipa sanaa zao ziwe na uhai zaidi.Katika kazi ya utafiti mtunzi huyu amehakiki matumizi taswira kubainisha maudhui katika *Utendi wa Al*

*Inkishafi.*Mtunzi ameyasheheni mazingira na historia ya Utawala wa WaOmani katika eneo la Pwani ya Afrika Mashariki.Mtunzi amefanikiwa kuonyesha picha kamili ya uharibifu wa malighafi wakati wa vita dhidi ya Waamu na utawala wa Sayyid Said karna ya 19.

Mtunzi ameonyesha picha halisi ya kuonyesha mporomoko wa miji kama Pate ambayo awali ilikuwa miji ya anasa na starehe.Ni katika Ubeti wa( 44-45) zinasawiri taswira ya mpomoko wa Pate kwa kina na kwa kuvuta nathari za msomaji yeyote.

*Ukwasi ungapo na tafakhuri*

*Wakanakiliwa ili safari*

*Ashukiye nyumba za makaburi*

*Mt'anga na fusi ziwafusiwe (U.44)*

*Sasa walaliye moya shubiri*

*Pasipo zuliya wala johari*

*Ikiwa miwili kutaathari*

*Dhiki na ziyara ziwakusiye (Ub.45)*

Ni wazi kuwa hisia na tanzia inayokumba miji kwa njia ya taswira inayoangaza mahame, magofu, na hata vifo vya wakwasi wa miji hiyo.

Kahigi (1973), katika ushairi wake uitwao *Jua la Dhahabu* shairi lizima linafaulu kutuandalia taswira ya jua lenye miale ya rangi ya dhahabu ipenyayo kote nchini.;

*Miale yake imepenya*

*Anga la nchi yangu*

*Na kukifuza kiza*

*Mbele ya macho yangu (Ub.18)*

Ni wazi kuwa miale anayomaanisha mtunzi ni nguvu na matumaini wa wanyonge kwa kufukuza kiza la kudharaul na kunyonywa na wakoloni enzi hizo za kabla ya uhuru wa Tanganyika.

## 1.9 MBINU ZA UTAFITI

Ni wajibu wa kila mhakiki kuchagua mbinu za utafiti atakazotumia kuhakiki kazi yake ili iwajibikie matakwa yake. Mbinu za utafiti zinaochukuliwa hutegemea mada la utafiti.

Sehemu kubwa ya utafiti wetu itakuwa ni ya maktabani.Kwa kuwa utafiti wetu ni wa fasihi andishi tutadurusu makala mengi yanayohusiana na Tendi na mashairi ya kiwasia. Aidha tutadurusu aina nyingi za vitabu, majarida, na tasnifu ambazo zimehakikiwa awali mradi ziwe ni kuboresha kazi yetu ya utafiti. Hatuna budi kunukuu wahakiki wengine, mradi kazi zao ziwe ni za manufaa kwa utafiti wetu.

## HITIMISHO

Katika sehemu hii ya sura ya kwanza ,tumezungumzia masuala ya kimsingi kama vile Usuli wa mada,tatizo la utafiti,madhumuni ya utafiti,nadharia tete,na sababu ya kuchagua mada yetu.Aidha tumeshunguza yalioandikwa kuhusu mada yetu,msingi wa nadharia,kuweka upeo na mipaka ya uchunguzi wetu. Madhumuni yasehemu hii ni kuweka msingi dhabiti wa utafiti wetu.

Katika sura ya pili, tutajadili masuala yanayomhusu mtunzi wa *Utendi wa Siiraji* kama vile asili yake, kuzaliwa kwake, elimu, ndoa na mchango wake katika fasihi ya Kiswahili.

## SURA YA PILI

## 2.0 MAISHA YA MTUNZI KIJUMWA

### 2.1 UTANGULIZI

Katika sura hii, tutatalii historia ya mtunzi na mchango wake katika nyanja mbalimbali za kiusanii.Lengo la sehemu hii ni kuweka uwazi kuhusu kazi za mtunzi ili kuzipa hadhi pia kulinganisha kiwango chake cha ubunifu na utendakazi wake kwenye Nyanja ya sanaa.

Ni bayana kuwa kila mtunzi huibua mawazo ya ubunifu na kuyaunganisha kwenye kazi yake ya usanii. Walakini dhana ya mtunzi inaweza angaziwa kwa jicho pana. Suala ambalo tunatazamia kubaini kana kwamba mtunzi ana mtindo fulani wa usanii wake.

Aidha tajriba yake imeathiri kazi yake kwa kiwango kipi. Aidha kwa kuangazia maisha ya mtunzi ,tutadondoa uhusiano wake na mazingira alimokulia na kana kwamba mazingira alimokukulia imeadhiri usanii wake kwa njia moja au njingine.

Matakwa yetu kuhakiki maisha asili na mchango wa mtunzi katika nyanja na viwango mbalimbali vyake vya kiusanii, ni kufidia maswali ambayo tungeibua akilini mwetu, na kupata msingi bora kuelewa kilichomchochea mtunzi katika kuandika kazi hii, mitazamo yake ya ulimwengu, hisia zake, umaarufu wake wa sanaa, na pia mihimili yake aitumiayo kupambana na changamoto za maisha ameikulia katika uwanja wake wa usanii.

Njogu (2008:480) anasema ya kwamba tunapozungumzia falsafa ya mtunzi, tunaibuka na maana ya falsafa ya kijumla ambayo hujionyesha katika masimulio yake yanayoakisi tajriba katika masimulio yake kwani tajriba yake imekuzwa na jamii yake.

Falsafa ya maisha ni jumla ya mtazamo wa mtu au watu kuhusu dhana ya maisha. Kulingana na kimani (2008:49) "falsafa ya mwandishi hutokana na utazamaji wa yale yanayojiri katika jamii yake, kisha akayatafakari akiwa pekee au na wengine na kisha kuitolea hukumu. Mtazamo wake utaadhiriwa na mazingira yaliyomlea na kumkuza''.

Maoni ya mhakiki huyu yameafikiana na mitazamo yetu kwani mazingira aliyekulia mwandishi yanaweza athiri mitazamo yake ya ulimwengu. Usimulizi wake aidha hujengwa na tajriba yake. Kwa kuhakiki historia ya mtunzi huwa tumeyakisi kwa kidokezo tu, jinsi athari ya mazingira yake yanavyomwathiri na kutawala kazi zake za kiusanii. Mfano mzuri ni wa Mwandishi na mtunzi Euphrase kezilahabi.

Msanii huyu ni maarufu sana kwa kazi zake za kiudhaishi. Kulingana na Sonja Mezger (2002), anasema kuwa msingi wake wa elimu ya upadri umeathiri kwa kiwango kikubwa sanaa yake ya uandishi. Falsafa ya dini ya Kikatoliki imesheheni kwa wingi katika kazi nyingi zake za fasihi. Aidha mtazamo wake wa maisha ya wahusika wake wakuu ni wa kitanzia na kukata tamaa.

Riwaya zake kama vile *Kichwamaji (1974), Rosa Mistika (1971) na Gamba la Nyoka (1979)* ni miongoni mwa kazi za kifasihi ambazo zina ushuhuda wa kuathiriwa kwake na imani na nadharia ya dini ya Kikatoliki. kwa kuwa na mtazamo hasi wa dini

hiyo ya Kikatoliki kwani alisomea Seminari na wala hakupata nafasi ya kumaliza kozi yake.

Kwa kurejelea malengo yetu, tutawajibika kumhakiki mtunzi wa *Utendi* wa *Siiraji* na kushabihi dhima yake ya uhalisia wa jamii, athari za mazingira alimokulia, athari ya elimu yake, utangamano wake na wanajamii na wageni Matakwa ya kumulika maisha ya mwandishi ni kuazimia uadilifu wa maandishi yake, sio tu kwa kumpa ujagina, bali ni. kapata ukweli wa kazi yake.

### 2.1.1 ASILI YA MTUNZI

Mtunzi tunayetolea maisha yake ni Muhammadi Kijumwa.

Jina lake kamili kinasaba ni Muhammadi Kijumwa bin Abu- Bakari bin Omar bin Abu- Bakari bin Othmani bin Muhammad Ali bin Muhammadi bin Omari, bin Muhammadi bin Abdalla bin Ibrahim bin Yusuf al- Bakari al- masihi. Ni katika *Utendi wa Siiraji* Ubeti wa 209 aidha unadhibitisha jina na ukoo wake mtunzi anaposema;

*Helewa twaa alam*
*Mekupa fundi kijuma*
*Bini bwana ikirama*
*Al- Bakariy Asiliya.*

Abou Egl. (1983) anasema kuwa babake aliyeitwa Sheikh Abu Bakr aliaga dunia akiwa mdogo na akalelewa na mamake Kamari au kwa jina maarufu (Mwana Kamari). Alikuwa *sharifa* (ukoo wa mtume Muhammadi ).

Kineene (2006) anasema kuwa jina la kwanza alilopewa na mama yake ni Kijuma (Juma au Ijumaa ndogo) na baadaye pia akamwita Muhammadi.

Mama yake Kamari ametajwa kwenye wasia huu Ubeti wa 44 anaposema;

*Bibi yako mwanake*

*Ni Kamari ina lake*

*Kulla siku kinambia*

**2.1.2 KUZALIWA**

Buttner (1894;78) anadai ya kwamba Muhammadi Kijumwa aliishi kati ya mwaka wa (1855- 1945) na alizaliwa na kulelewa eneo la Lamu pamoja Pate na viunga vyake.

Mwaka wa kuzaliwa kwake mtunzi umenukuliwa kwenye karatasi yake aliyowasilisha mtafiti Olali kwenye kongamano la kitaifa la 6 la Lamu (2006), kuwa mtunzi alizaliwa mwaka 1855 na kuaga dunia akiwa na miaka 90, kabla ya kumalizika kwa vita ya pili vya dunia.

Maoni haya yana mwelekeo sawia na ule wa watafiti wengi wa fasihi za Kiswahili. Kwa maoni haya tunaweza kudai kwamba Kijumwa alizaliwa kati ya mwaka wa (1855-1945) kulingana na maoni ya wahakiki wengi.

Ni bayana kuwa maisha yake yalikumbana na wakati wa majilio ya watawala wa kikoloni, wanabiashara wa kigeni waliofanya biashara ya watumwa maajilio ya wamishenari Afrika mashariki na bara nzima kwa jumla.

Mtunzi alishuhudia mikabala ya utawala wa Waarabu na Wakoloni wa Ureno, Uingereza ambao walitawala kati ya miaka yake ya kukua.

**2.2 ELIMU YA MTUNZI**

Kama vile tulivyokuwa tumetaja hapo awali, Mtunzi alikuwa mzaliwa wa Lamu. Lahaja ambayo inazungumzwa Lamu ni ya Kiamu. Kisiwa cha Lamu kiliitwa zamani "kisiwa cha ndeo." Fasili ya dhana hii ni cha ' *Kisiwa cha Majivuno'* Mohamed S.A 1995).

Lahaja ya Kiamu ilisawiriwa kama lahaja ya wasomi kwani tendi nyingi ziliandikwa kwa lahaja ya Kiamu hasa katika karne ya 19. Sehemu hii ya Lamu ilizuka watunzi wengi wa kimashairi maarufu ambao walibuni tungo zao kwa lugha za Kiamu.

Watunzi walioimarika zaidi ni kama Muyaka bin Haji (1776-1840), Sayyid Abdalla bin Nasir (1718-1815), mtunzi wa *Utendi* maarufu *Al-Inkishafi* na Mwana Kupona Binti Mshamu, na wengineo. Mtunzi alilelewa katika mazingira ya watunzi wa fasihi simulizi na andishi walikuwa wamesomea mashule yaliomilikiwa na dhehebu la dini ya Uaislamu nayo *Madrassa.*

Mazingira ya mtunzi alimolelewa na kukulia yalikuwa ya kiusomi na ya wasomi wenye kutalakiwa. Olali katika wasilisho lake katika kongamano sita "*Lamu Cultural Festival*", anasema kuwa mtunzi alipitia masomo ya *madrassa* na tangu utotoni alikuwa mwenye kipawa cha kunakili na kubuni mada alizopewa \ na hata kubuni zake mwenyewe.

Aliweza kunukuu sura nyingi za *Qu'ran Takatifu* na kuandika kwa kasi sana kwa hati za Kiarabu. Alice Werner (1934) anaelezea kuwa mtunzi alikuwa na kipawa cha kufasili lugha nyingi kwani alikuwa na umahiri wa kutafsiri kazi nyingi za Kiarabu, Kirumi na kwa lahaja za Kiswahili bila shida nyingi.

Ni bayana kuwa hata kama historia ya masomo yake haijaangaziwa kwa undani, ni dhahiri kuwa mtunzi alikuwa na umilisi wa masomo aliyopata kwenye vyuo vya *Madrassa* kwani utaratibu wa masomo ya vyuo kama hivi vinatanguliza kusomesha na kuelewa kuandika kwa hati za Kiarabu.

Ni vyema kugundua kuwa masomo ya kikweli sio tu yale rasmi ya vyuo, bali elimu na hekima huongezeka kwa tajriba, maingiliano na watu na mazingira kwa ujumla.

Ni bayana kusema kuwa motisha hupatikana wakati mtu anapofanikiwa kutatua shida zake zinazomkumba yeye mwenyewe.

*Madrassa* yalikuwa vyuo vya kukidhi, kupanua imani na itikadi yao, kulingana na mafunzo ya *Qu'ran Tukufu*. Hivyo ni kumaanisha kuwa silabasi yao ilijikita kwenye mafunzo ya *Qu'ran Tukufu*.Wahakiki wa kigeni waliotamani kuandikia na kuhakiki fasihi za Uswahilini ambazo zilihifadhiwa kwa hati za Kiaarabu, iliwabidi watafsiri tungo hizo kwa hati walizozielewa za Kirumi. .Miongoni mwa wakuza misuada na watafsiri waliojulikana zaidi ni Muhamadi Kijumwa.

Mtunzi huyu aliwafaa Maimamu na walimu wa dini ya kiislamu kwa kuwatafsiria kazi na fasihi zilizoandikwa kwa hati ya Kiarabu na kuibuka msomi sugu tangu ujana wake. Waliosoma walisawiriwa kuwa wenye maendeleo waungwana na wa hadhi ya juu zaidi miongoni mwa jamii yao. Aidha mtunzi alianza kuwatungia vitabu vilivyotumiwa na Maimamu kufundishia dini ya Kiislamu eneo nzima ya Lamu, (Edward Steere, 1870).

## 2.3 ASASI YA NDOA

Asasi ya Ndoa husawiriwa kama kigezo cha ukamilisho wa usuhuba. Muungamo huu wa mume na mke huwa ni kipaji cha kihiari cha pande zote mbili, kwani wao

hudhamiria kuanza safari ya kuishi pamoja kama mme na mke. Laylon (1978) anatathmini "ndoa kama njia moja ya kutimiza matakwa ya jamii wanamoishi, kwa kutimiza uhusiano baina ya mume na mke na pia kuhalalisha watoto.

Kamusi ya karne ya 21 Longhorn (2011:383) inafafanua ndoa kama "maafikiano rasmi baina ya mwanamke na mwanamme. Bila shaka ndoa ni umangamo ya kudumu kati ya mme na mke.

Desai, (1981: 282) anafafanua nikaah kama, dhibitisho ya kuafikiana kati ya mume na mke.

Upatanisho huo huwaepusha kufanya dhambi na ndio njia kuu ya kulea familia na kuendeleza mfumo wa asasi ya ndoa inayosahili, isiozini na yenye kiunzi cha usafi wa jamii inadumisha maadili mema.

Maoni ya waandishi hawa ni ya kimsingi kuhusu dhana ya ndoa, kwani hakuna ndoa inayoweza kukubalika bila masharti fulani yatakayowekwa kati ya mume na mke. Tutawajibika kuangazia ndoa ya Ukristu, Uislamu na kwa mujibu wa sheria za nchi ya Kenya.

## 2.4 NDOA KWA MUJIBU WA SHERIA ZA SERIKALI YA KENYA

Ndoa hujitokeza kama taasisi inayokubaliwa na tamaduni zote ulimwenguni. Kimondo (1997) anaelezea na kuchanganua aina nne za ndoa zinazokubaliwa kisheria nchini Kenya na inayowakilishwa kwenye *Katiba* ya Kenya kwenye kipengele cha 45 Haki ya familia. Nazo ni ndoa za Kiutamaduni, ndoa kwa mujibu wa sheria za Kiislamu, ndoa kwa mujibu wa tamaduni za Kihindi na ndoa kwa mujibu wa sheria za kiraia (civil marriage).

Tutazihakiki ndoa aina mbili ya kikristo na kiislamu kwani ndizo zinazochukua mikabala sawia na dhamira ya mtunzi wa *utenzi* tunaouhakiki, kama itakavyodhihisha baadaye.

## 2.5 NDOA YA KIISLAMU

Busaidy (1958) Anawazia kuwa ndoa au *Nikahi* ni jambo linalohimizwa katika *Qu'ran Tukufu* na mwenyezi Mungu kama inavyodhihirika katika Sura ya 4 aya 3 inayosema "Oeni wanawake wanaokupendezeni..."

Al-Jawad *et-al (*2008) anaelezea kuwa ndoa za kiislamu ni sharti ziwe halali. Ndoa hizo ni zile zenye masharti ya Nikaha kama vile; kuoa wanawake wasiozidi wanne, mume kumchagua anayempenda kumwoa, na ni kinyume kumwoa mtu wa nasaba yako, kuolewa kwa halali za dini ya kiislamu. Maoni ya mwandishi huyu yanawazia kuwa ndoa za Kiislamu hufuata kaida na sheria Fulani zilizowekwa na kukubaliwa na waumini wa dini ya Kiislamu.

Busaidy (1958) anafafanua kuwa ndoa haramu ni ile ndoa ya ***shighar*** yaani ndoa ya "kubadilishana" watoto bila kuzingatia mahari wala kulipana kati ya pande zote mbili. Ousmane (1972), anadokeza kuwa kwa muda mrefu jamii ya Waswahili imeunda itikadi mahsusi chini na kwa misingi ya dini ya kiislamu na ya kwamba hata zile zinazobainisha kujamiana kwa watu wa *akraba* (ndugu wa karibu) moja zinachukuliwa kwamba zimepangwa na Mungu.

Mawazo ya mhakiki huyu yanakaribiana na misingi ya ndoa zote kwa sababu hutilia mikazo kudura na neema ya Mungu ndiyo inayofanya ndoa ifaulu.

Ndoa ya kiislamu imekubali mme kuoa wanawake wane pekee na wala sio zaidi ya hawa kulingana na *Qu'ran Tukufu* Sura ya 4;3. Imemtahadharisha mme kutozingatia familia yenye ubora.

*Utendi* tunaouhakiki umesheheni swala la ndoa na imethibitishwa kwenye ubeti wa 169 pale ambapo mtunzi anamshauri mwanawe Helewa kuakisi ndoa timilifu huku akinukuu *Qur'an,( sura: 69).*

**2.6 NDOA YA KIKRISTU**

Ndoa ya Kikristo ina misingi yake ya kimagharibi. Ndoa ya kikristo ina mihimili mizito kwenye mafunzo ya *Biblia Takatifu.* Ndoa ya kwa kwanza iliasisiwa na Adamu na Hawa pale shamba la Edeni, iliyoungamwa na kusimamiwa na Mungu mwenyewe.

Nikahi ya kikristo huhalalisha ndoa ya mume na mke mradi ikubaliwe na familia zote mbili

Kimondo (1997:58) anadai kuwa Ndoa ya Kikristu haimruhusu mume kuoa wake zaidi ya mmoja, wala mke mlie na uhusiano wa kinasaba. Mme anayeoa sharti awe ametimiza wajibu wa kitamaduni kama vile, kulipa mahari, na kuidhinishwa na aila ya pande zote mbili.

Idhini ya wazazi wa pande zote mbili ni muhala na nikahi ya kikanisa ndiyo kitambulisho cha ndoa ya kikristo. Mume na mke hula kiapo na hubadilishana pete kama ishara ya fungate za kudumu na kuaminiana hadi kifo kitakapowatenganisha.

*Biblia* inadhinisha mwanamme kumwoa mwanamke mmoja katika kitabu cha (*Waefeso 5: 22*) jinsi mume na mke wanavyostahili kuishi kwa umoja na upendo na

*"kama vile Yesu alivyoipenda kanisa"*. Hii ni dhihirisho ya kuonyesha ndoa inahimiza mke na mme kuaminiana milele. Endapo kutoaminiana kutazuka, hapo ndipo talaka hutolewa kwa mjibu wa sheria za nchi husika

Kusudio letu la kufasili aina hizi za ndoa ni kwa sababu hata kama ndoa zake hazikudumu mtunzi ameliwaza dhana ya ndoa kwenye utendi tunaouhakiki. Mtunzi amesisitiza wazo la kuungana kwa dhati kati ya mume na mke anaposema;

*Mke wako mpumbaze*

*Kwa uwezalo mweneze*

*Na wewe simtele*

*Nde ukalimatiaUb.171*

## 2.6.1 MAISHA YA NDOA YA MTUNZI

Abou Egl, (1983) anaelezea kuwa mtunzi ameoa wanawake watatu maishani mwake. Mke wa kwanza aliitwa Maryam. Mkewe wa kwanza hawakuishi naye kwa muda mrefu. Mtunzi alimpa talaka baada ya kudai kuwa aliyapuuza na kuyaacha masomo ya Dini ya *Uislamu* iliyokuwa ikisomeshwa misikitini. Kulingana na maoni ya Mhakiki huyu, hawakufanikiwa kupata mtoto yeyote na mke huyo.

Mke wa pili aliyemwoa alikuwa Fatuma binti Ali Kitole aliyekuwa maarufu kwa jina la "*Kinana*" au (*nana mdogo)*, katika mwaka wa 1885. Nasaba ya Mke huyu ilitokana na familia iliyokuwa mahirika ya Al- Mahdaliy. Alimpa talaka mke huyu wa pili kabla ya mwaka wa 1900. Walifanikiwa mtoto mmoja pekee aliyeitwa Ali, maarufu sana kwa jina Helewa. Asili ya jina helewa ni "*Halua*" ambacho ni chakula laini na kitamu kinachotengenezwa kwa unga, mafuta na sukari. Helewa alizaliwa mwaka wa 1885 na kuaga mwaka wa 1951 akiwa na miaka 66.

Helewa alikuwa maarufu sana katika kazi ya useremala hasaa ya kutia nakshi vifaa vya mbao na kuunda sanamu za mawe. Kuna mifano ya picha ya baadhi ya kazi za usanaa walizozifanya na babake.Helewa ndiye aliyemfundisha rafiki wake wa karibu bwana Skanda Abdalla na mchongaji maarufu katika upwa wa Afrika Mashariki.

Mke wa tatu wa Kijumwa aliitwa Esha bintiye Khatibu na nduguye Ahmadi. Aliishi na mwanamke huyu kwa miaka mitano.

Kwa kulihali ndoa ya mtunzi ,tunashawishiwa kutoa maoni kwamba mtunzi ametilia maanani ushauri wa kufanya ndoa iwe dhabiti kwa kuandika Utenzi kudumisha uhusiano wa karibu kati ya mume na mke kwa sababu labda alihofia majanga ya ndoa ya kutalikiana yasimjie mwanawe wa kiume na wa pekee.

## 2.7 MCHANGO WA KIJUMWA KWENYE UWANJA WA FASIHI

Mchango wa mtunzi katika uwanja wa fasihi ni wa kipekee.Mtunzi alipata umaarufu kwenye uwanja wa sanaa ya fasihi ya uandishi na pia wa masimulizi; kwani alikuwa mtungaji wa Tendi, mashairi, nyimbo, mkuza miswada, mwanamziki, mutribu, nguo, mwigizaji mtafsiri, seremala, mshona fundi wa ala za mziki, mchongaji, mcheza densi maarufu na mchoraji wa kutamanika.

Werner (1934) anawazia kuwa hakuna mtunzi wala mkuza miswada aliyechangia, kufanikisha na kunawirisha fasihi ya Kiswahili kuliko Muhammadi Kijumwa wakati wa enzi zake.

Abou Egl (1983) anaelezea kuwa mtunzi alifanikiwa kutunga, kuandika, kutafsiri, kuhariri na kukusanya kazi mbalimbali za fasihi ya kiswahili ambazo zimejikita kwenye makundi *manne*. Nazo nii:

i) Kazi alizozitunga mwenyewe na kuwanukulia wataalamu wa kigeni kwa hati za Kirumi.

ii) Kazi alizozitunga mwenyewe lakini akatia majina ya watunzi wengine au akawaeleza wataalamu wa kizungu kwamba watunzi hawajulikani, kwa sababu ya hali yao kiuchumi, kisiasa wa kidini.

iii) Kazi alizozitafsiri kutoka kwa kiarabu na baadaye kuzinukuu.

iv) Kazi alizozitafsiri kutoka lahaja ya kimvita hadi ya kiamu.

## 2.8 KAZI ZILIZOTUNGWA NA KIJUMWA MWENYEWE NA KUWANAKILIA KWA HATI YA KIRUMI WATALAAMU WA KIGENI

Knappert (1967) anaelezea kuwa mtunzi alitunga tungo zake kuhusu takribani kila kitu. Alibuni tungo kutoka hadithi za *Biblia Takatifu* na pia kwa *Qu'ran* Takatifu. Mawazo haya tunayaunga mkono kwani tungo tutakazozirejelea ni tungo zenye bunifu za kutamaniwa na wengi kwa ueledi wa kufinyanga lugha na kuibua fasihi yenye mafunzo ya falsafa ya juu.

*Utendi* wa *ndiwa na kozi* ni utendi maarufu ambao una mafunzo ya kuwa tusishawishiwe na matendo yasiotufaidi. Utendi wenyewe ni wa kimajibizano baina ya *Nabii Musa,* malaika *Mikaili* na *Jibrili a*mbao wamejifanya *kozi* na *njiwa* (aina za nyuni) *Utendi* huu ni wa beti 37.

Utendi ambao ni maarufu sana wake ni *Utendi wa Fumo Liyongo* alioutunga mwaka wa 1913. *Utendi* huu ni maarufu na unasimulia sira ya ujagina wa *Liongo Fumo.* *Utendi* huu una maudhui ya migongano ya wenyeji na utawala wa Kisultani Aidha

umesawiri mifumo ya kijamii.Utendi huu umehaririwa na wahakiki wengi akiwemo Hichens, Allen na Werner.

*Utendi* wa kisa cha na *Haramia na Kadhi / Kadhi na Haramiya* beti (234) utendi huu umetungwa, mwaka wa (1914) na kunakiliwa na Yahya Ali Omar. Utendi huu ni maarufu kwa misingi yake ya kutathmini nguvu za ushawishi wa shetani na hatimaye kuangazia nguvu na uwezo wa Mungu. Aidha maoni ya Dammann (1957:432) Yanaafikiana na tafsiri yetu anaposema kuwa mtunzi anatueleza jinsi kadhi alivyokabiliana na mwizi aliyetaka kumnyanga'nya vazi lake, huku kila mmoja akikariri aya kutoka *Qu'ran Takatifu* la hila na makusudio yake ya kitendo chake.

*Utendi* wa *Mwana Kupona* una beti 198 zile alizonukuu yeye na mwana kupona binti mshani mwake wa (1858). *Utendi* huu sii kazi yake bali aliunakili kutoka kwa hati za kiuarabu hadi kwenye lugha Kirumi.

*Utendi wa Yusufu* ulitungwa mwaka wa 1913. Asili ya hadithi yenyewe ina misingi ya vitabu vitakatifu vya *Qu'ran* Tukufu na *Biblia Takatifu*. Katika Biblia hadithi inapatikana kwenye *Agano la kale.*

*Utendi* wa *ngamia na paa* na *Utendi* wa *Mkunumbi* ni miongoni mwa tenzi aliweza kuzinukuu mwenyewe.

*Utendi wa miiraji* (beti 664). Utendi huu ni maarufu kwa wafuasi wa dini ya kiislamu. Unahusu safari ya Mtume Muhammadi kutoka Mecca, Yelusalemu, hadi mbinguni.

*Utendi wa mkunumbi* ni baadhi ya tendi alizoandikia watunzi wengine na kuwatafsiria wageni. Ulitungwa 1913 *Utendi* huu ni mojawapo ya tendi alizowatungia wageni na

kuwajulisha kuwa watunzi wa tungo kama hizo hawakujulikana kwani yeye hakutaka kujihusisha na siasa.

## 2.9 KAZI ZILIZOTAFSIRIWA NA KIJUMWA NA KUZINAKILI KUTOKA HATI ZA KIARABU HADI KWA HATI ZA KIRUMI

Mtunzi alinukuu na kutarjumi kazi hizi kutoka hati za Kiarabu hadi Kirumi. Nia iliyokuwako kushughulikia Tendi nyingi za kikale, ni kuwa Tendi nyingi zilikuwa maarufu sana baada ya kutafsiriwa kimaudhui na hivyo kuwapa msukumo na mutisha wa kutafsiri kazi zingine.

*Al- Inkishafi* ni Utendi maarufu sana umetungwa na Abdalla bin Nassir (1720-1820) na ambao una beti 79. Utend*i* huu Umetolewa Misuada mitano na wahakiki wafuatao; Hichens (1972), J. Allen (1977), R. Allen (1946:243-249) Harris (1962:86-102) na Wamlamali (1980).

## 2.10 KAZI ALIZOZITAFSIRI KIJUMWA KUTOKA KIARABU HADI KIAMU NA BAADAYE KUZINUKUU

Tendi hizi ni miongoni mwa tendi alizozitafsiri kutoka hati za Kiarabu hadi kwenye lahaja zingine katikati na mwisho wa karne ya 19;

***Siri li Asirari***

***Wajiwaji***

***Kasida ya Burda***

***Utendi wa Fatuma***

***Kahifu***

***Takhmisa ya liyongo***

***Hezekali /Utendi wa Hirgal.***

***Utendi wa Ayubu.***

*Utendi* wa *Qatirif. Utendi* huu ulitungwa na Abu Bakr bin Mwengo na ukanakiliwa na Muhamadi kijumwa.

**2.11 NYIMBO ZILIZOTUNGWA NA KIJUMWA**

Kulingana na maoni ya Knappert (1967) mtunzi amewahi kutunga nyimbo za nikahi na za tumbuizo. Nyingi yazo zilitungwa kati ya mwaka wa (1700-1800). Nyimbo zake zilitangulizwa kwa kuporomosha midundo ya ala za mziki kama vile *ngoma* na *pembe*.

Olali (2006) katika wasilisho yake katika kongamano ya Lamu ya sita anasema ya kwamba mtunzi aliongoza kikundi kimoja maarufu cha densi ya kiutamaduni kilichoitwa *Beni*. Kikundi chake cha ngoma za kienyeji ndicho kilichoshinda mara kwa mara kwenye mashindano na hafla za nyimbo na densi za kiutamaduni miongoni mwa jamii ya Waswahili.

Aliwahi kutunga nyimbo zenye mada ya umuhimu wa wazazi kuwapeleka watoto shuleni. Yumkini nyimbo ambazo alizitunga kuhusu umuhimu wa elimu zilikuwa kichocheo kwa wale viongozi wa kiislamu, *Maliwali na Maimamu* ambao waliwakataza jamii ya Waswahili kuwapeleka watoto wao kwenye shule za mfumo wa ulaya na kupendekeza wasomee madrassa kwani mfumo huo ulilingana na mafunzo ya dini yao. Wao waliyofia watoto wao wakengeushwa na mila na desturi ya wakoloni.

## 2.12 HADITHI

Mifano ya hadithi alizotunga ni *Hadithi za watoto wanne (Betizo) Ushuhuda*. Hadithi ya *Miiraji* ambayo imeandikwa kwa mkono haijulikani ilitungwa lini. Dammann (1940) anadhibitishia kuwa kisa ambacho kimeandikiwa hadithi hii ni nukuzi za *Qu'ran Tukufu*. Hadithi zingine ni zile alizonukuu kutoka lugha ya Kiarabu na kuziandika kwenye lugha zingine kama vile Kireno na kwa lahaja za *Kiamu na Kimvita* Kiswahili. Hadithi hizo ni miongoni mwa zingine kama; *Hadha Kissat al-Kadhi Ma'ah al-Haramii.*

## 2.13 TUTUMBI NA BARUA

Abou Egl, (1983), anaelezea kuwa mtunzi amewahi kuandika biografia ya Sheikh Mohamed Makata na Sultan Ahmadi. Mswada huu ulipewa mtafiti Alice Werner na baadaye kumkabidhi mtafiti mwingine wa fasihi za Kiswahili aliyeitwa William Hichens huku ukiwa kwenye hati za Kirumi. Mswada wenyewe ulikuwa kwa hati za kiarabu walakini na mtunzi aliweza kuunakili kwa hati za Kirumi.

Aidha aliwaandikia watafiti wa fasihi ya Kiswahili barua kuhusu kusanyo zake kwa hati za Kirumi. Miongoni mwa watafiti wa kizungu aliowaandikia ni; Hichens Williams, William Taylor, na Ernst Dammann. Barua nyingi zilihusu masuala ya utafiti wa fasihi, historia ya Kiswahili na kusanyiko za mashairi ya Kiswahili hasa ya eneo pwani ya Mashariki.

Waraka nyingi zilikuwa kati yake na Hichens ni mmoja wa wale walionufaika sana kwa kusanyo na miswada mingi ya fasihi ya Uswahilini. Kulikuwako na barua chache alizoandikiwa na Bwana Whitton, *wakala* wa forodha na ambazo zilihusu kusafirishwa kwa miswada na kupokea chochote alichotumiwa kutoka uingereza

pahali miswada ilitumwa. Kuna barua tatu kati ya Hichens na mtunzi akimushukuru kwa miswada na maelezo ya *Utendi* wa *Hamziyya, Utendi wa Ayubu, Utendi* wa *Liyongo*, *Al- Inkishafi* na *Hadithi* ya *Barasisi* kwani maelezo ya miswada hiyo iliwafaa na kurahisisha kuelewa maudhui na lugha iliyobuniwa kwenye tungo hizo.

## 2.14 KAZI ALIZOTAFSIRI KUTOKA KWA LAHAJA MOJA HADI NYINGINE

Aidha alimtafsiria William Taylor kitabu cha Biblia kiitwacho, *The Gospel of St. John* (Krs. 72) kutoka lahaja ya Kimvita hadi ya Kiamu.Huenda kulikuwa na tafsiri nyingi alizozifanya kutoka kwa lahaja moja hadi nyingine walakini hazikuwekwa kwa kumbukumbu za wahakiki au labda hazikuwa za manufaa kwa wao.

## 2.15 UHUSIANO WA MTUNZI NA WAGENI NA WANAJAMII

Ni bayana kusema kuwa uhusiano kati ya mtunzi na wageni wa Kizungu, Wakiarabu na wamishenari ulikuwa wa juu wa kirafiki na pia wa kitaaluma. Uhusiano wake na watafiti wa fasihi ya Kiswahili ulizaa matunda ya kutambaa kwa fasihi ya Kiswahili barani Afrika na ulaya kwa ujumla.

Maingiliano yao yalikuzuka kwa sababu ya ueledi wake wa kutafsiri miswada kutoka lugha moja hadi nyingine, na ushabihi kweli na wanajamii wenzake aliyokusanya fasihi simulizi kutoka kwao. Mtunzi alikuwa kielelezo cha watunzi eneo lote la pwani kati na mwisho wa karne ya 19 na mwanzo wa karne ya 20.

Aidha ni vyema kutambua maingiliano yake na watafiti wa kigeni kwa njia za waraka .Hii ni dhihirisho kuonyesha kulikuwako na urafiki kati yake na watafiti hao

wa kigeni. Mtunzi alikuwa msaidizi wa karibu W. Hichens. Mtunzi alimkusanyia kazi nyingi za kifasihi hususani za *Historia ya Kiswahili* ya eneo la Lamu na viunga vyake. Alikuwa na uhusiano wa dhati na Liwali wa Lamu, Saif bin Salim wakati wa enzi yake.

Walakini mtunzi hata kama walitangamana na wazungu, waarabu na wageni wamaeneo mbalimbali ya ulimwengu, hakudhubutu kukengeushwa na tamaduni na mikabala ya kigeni. Mtunzi aliwahi kujihusisha zaidi na utamaduni wa Waswahili hasa wa kiamu na kukwepa mambo ya siasa.Haimaanishi alikuwa kibaraka wa wazungu bali alitamani kukaa maisha ya furaha na ya ucheshi. Mitazamo ya kiutamaduni inajidhihirisha kwenye tungo alizobuni zilizosheheni masuala mazito ya utamaduni wa waswahili yaliyoangaziwa kwenye sanaa yake ya fasihi andishi na simulizi.

## 2.16 USANAA WAKE KATIKA NYANJA ZINGINE

Sanaa yake kando na fasihi ilikuwa hodari na ya kutamaniwa. Mutunzi alikuwa mchoraji, mwanakaligrafia (*taalamu ya uandishi*), seremala hususan wa kutia nakshi vifaa vya mbao, mawe na vyuma. Aliunda ala za mziki kama vile *Kibangala* kwa njia ya uchongaji na uchongaji wa aina nyinginezo za sanamu.

Kati ya usanii ambao uliridhiwa na aila yake ni ule wa sanaa ya uchongaji na kutia nakshi katika vifaa vya mbao na mawe. Mtunzi tunayehakiki ndiye mtu wa kwanza kutengeneza na kutumia *kinanda* au ***gambuzi*** eneo Lamu.

Olali (2006) anadai kuwa mtunzi ndiye aliyekuwa mtu wa kwanza kutunga na kutayarisha ngoma *ya mwasha* na *kinanda.* Tukirejelea yale ambayo tumeyatalii, mtunzi aliwahi kufunza mtoto wake wa kiume, Helewa, kozi ya useremala. Helewa aliwajibika katika kozi hiyo na kuwa stadi katika kuweka nakshi vifaa vya mbao iwe ni milango ,jahazi, vifaa vya nyumbani na kuweza kuvuma eneo la Lamu ,Pate, Zanzibari , Mombasa na pahali pote alipoangia.

Milango ya Wa Omani ambayo ilikuwa maarufu kwa kaligrafia ya nakshi ikawa kazi ya kifahari wa watu wote, kwani aliiga usanii huo na kuunda milango sawia na hiyo. Ndiposa kukazuka milango ya *Waswahili* wa Lamu. Mfano ya mlango wa Lamu waliotia nakshi za kiusanii umetolewa picha halisi kwenye ukurasa wa 48.

Hatuwezi tukasahau kutoa sifa kwa mwanawe Helewa kwani aliwajibika na kufahamika kwa uchongaji wake wa kuweka milango nakshi na kazi yake ni maarufu mpaka wa leo.

Helewa kama babake alirembesha majahazi, na kuta za majumba ya *wangwana* yaani watu wa hadhi ya juu huko Unguja, Lamu, Pate na Mombasa na viunga vyake. Mwanafunzi wake wa karibu ambaya aliweza kuendeleza kozi yake anaitwa Abdalla Skanda. Alikuwa mahiri kwa sanaa hiyo ya uchongaji wa nakshi. Skanda et al ndio walioweka nakshi ya uchongaji, Lango kuu la *Mbunge ya Kenya*, jijini Nairobi katikati ya karne ya 20. Hatuna budi kutambua kazi ya mtunzi iliyoridhiwa na vizazi vingi mpaka wa leo.

## 2.17 IMANI NA DINI

Hakuna ushahidi wa kutosha wa kuonyesha kuwa mtunzi alikuwa mkristo, ingawa inasemekana kuwa alibatizwa na kuitwa **Masihi**. Mtunzi alizikwa kwa kaida za Kiislamu. Allen (1971).anasema kuwa

Kuna dhibitisho mtunzi aliwahi kuhiji Mecca na kuishi miaka themanini kama Mwislamu, Huku tukitoa uamuzi wa mwisho kumhusu mtunzi hatuwezi tukasahau kusema ya kuwa mtunzi alikuwa mwanafunzi na mpwa wa Sayyid Mansabu Abu Barari bin Rahmani, ambaye alikuwa mshairi maarufu wa dini ya Kiislamu.

Aidha kulingana na tungo zake hakuwa mlokole mwingi wa dini ya kiislamu.Tunashawishiwa kuunga mkono mwandishi Shaaban (1967;89) anasema kuwa tabia ya mtu hukolea kwa kazi yake. Shairi lake liitwalo "*natoa mawaidha inayo tabia*" kwenye diwani yake iitwayo *Pambo la lugha* ni ushuhuda wa kina tunapowazia kazi na maisha ya mtunzi Kijumwa , anapotunga na kusema kuwa;

***Tabia na mazoea,***

***Ni vitu vilivyo ndugu,***

***Hutufanya maridhia,***

***Ama konde la magugu,***

***ni kama mbegu inapopandwa humea.ub.1***

Tunakosa maneno ya kumtunukia mtunzi huyu wa kifahari ila yale yaliyosemwa kwenye ubeti tuliyounakili wa mtunzi Shaaban Robert.



**Mtunzi Muhammadi Kijumwa Abubakr akicheza ala ya Kibangala aliyounda.**



**Mfano wa kutia Nakshi za kimapambo kwenye Jahazi .**



**Mlango wa Lamu**

## 2.18 HITIMISHO

Kwa kuangazia historia ya mtunzi tumeimarika na kupanuka akili kuhusu mtindo anaouzoea kutungia tungo zake, mikabala anayoichukua, na pia tajriba aliyo nayo. Tajriba ni kama utajiri wa kila mtunzi kwani humsaidia kubuni na kuandikia mada tofauti anazoibua na zikawa za kusisimua wasomi au hadhira inayohusika.

Dhana ya dini imetiliwa mkazo kutia mkazo katika tungo nyingi zake kama *Utendi* wa *Musa na Firauni* , *Utendi wa Yusufu, Utendi wa Aisha na Muhammadi* ambao una nukuzi kutoka kwa vitabu vitakatifu vya *Biblia* na *Qu'ran Tukufu. Utendi* wa *Aisha na Mohammed* ambao amenukuu aya za *Qu'ran Tukufu* na kwa hivyo hakuegemea, dini moja pekee ya *Uislamu* kubuni hadithi zake ,bali aliweza kubuni kutoka kwa chanzo tofautitofauti

Tumegundua kwamba *Tendi,* mashairi na nyimbo nyingi aliweza kuzinakili kwa niamba ya watunzi wengine ambao hawakuwa na ujuzi wa kuandika kwa hati za Kirumi.

Miongoni mwa watunzi walionakiliwa kazi zao wenye asili ya Kiafrika ni Mashairi ya Bwana Bakari bin Mwengo ambayo yalinakiliwa kwa hati ya Kirumi. Inamaanisha kuwa mtunzi alikuwa mkarimu na mtu mwenye utu kinyume na wale watu wanaoonea wenzao gere.

# SURA YA TATU

## 3.0 UTANGULIZI

Sura ya tatu, ina migao minne mikuu. Tumeshughulikia dhana ya ndoa katika sura ya pili, walakini hatukudondoa misingi na dhana ya talaka ambayo ni muhimu kuielezea. Ndoa na talaka zina uhusiano, kwani masuala yote mawili yanahusu familia na jamii Ndoa ni muungano wa mume na mke kama tulivyokuwa tumetaja hapo awali, ilhali talaka ni utengano wa hawa wawili kwa mjibu wa utamaduni, mbeko au kwa mujibu wa sheria za serikali husika au za dini.

Dhana ya maadili au uadilifu ni suala ambalo tunakusudia kuingazia katika sura hii. Uadilifu kwa namna moja au nyingine huakisi misingi ya mitazamo ya jamii husika. Kila jamii ina mitazamo yake ya kimaisha ambayo huwiana na maisha yao, matarajio na jukumu na utekelezo wa kila mtu wa maisha yao kila siku.

Wamitila ((2008) anawaza kuwa, maadili ni uchukulio wa kila mtu katika jamii na uhalisia wa maisha ya kila siku. Tutafasili suala la taswira. Kigezo hiki cha taswira ni muhimu katika uhakiki wetu kwani ndio utakaokuwa msingi wetu wa utafiti. Katika uhakiki wetu tunadhamilia kudadisi vigezo vya taswira na jinsi taswira inavyoweza kuwa silaha ya mwandishi ili kuzinata akili za hadhira yake.

## 3.1 DHANA YA TALAKA KWA MJIBU WA DINI YA KIISLAMU

Tunashawishika kutoa fafanuzi za talaka kwa mjibu wa dini ya Kiislamu kwani ndio imeasisiwa kwenye *Tendi* nyingi za kimapisi kama vile *Kiokozi cha Banati Al Inkishafi*, Al na *Utendi* wa *Mwanakupona.*

Katika maisha ya ndoa hakuna kitu kinachoudhi kama talaka. Watu ambao huadhirika sana kuliko wote ni watoto ambao huwa wana uzoevu wa wazazi wote wawili. El-Busaidy (1958), anafasili kuwa *talaka* ni "hali ya mme na mke kuachana yaani kutalikiana na kutengana kwa mujibu wa sheria". Huku akinukuu kisa cha Mtume Mohammed kwenye *Hadith* Mtume anasema kuwa "*katika halali zenye kumchukiza mwenyezi Mungu ni Talaka.*"

Neno *talaka* lina asili ya jina la kiarabu '*Talak'* maana yake ikiwa kuachana kwa mume na mke katika ndoa.

Baada ya mtu kumwoa mwanamke kwa namna iliyokwisha elezwa katika dhana ya pili, tumeonelea tushughulikie dhana ya talaka kwani mtunzi wa *utendi* tunao ushughulikia amelitilia maanani kwa upana. Kwa mfano katika.

Mtunzi anamshauri mwanawe wa kiume na wa kipekee Helewa na mchumba wake jinsi watakavyoshughulikia la kutalikiana anaposema ;

***Na siku ya kukwambia***
***Niwata nawe ridhia***
***Ni kheri kuitokea***
***Ama utaiyutia. Ub.172***

Kulingana na mila na desturi za waswahili talaka inapeanwa kwa misingi ya dini na sheria za Kiislamu. Tutaliangazia suala la talaka kwa mujibu wa dini ya kiislamu kama tulivyokuwa tumetaja hapo awali. Talaka imehadithiwa kwa urefu katika Sura ya 65;1-6 kwenye *Qu'ran Tukufu* na kusema "*hapana budi au njia nyingine, basi ni haki na ni lazima itokee".*

Dini ya kiislamu inakachifu mno watu walioko kwenye asasi ya ndoa kugombana na kuudhiana, kwani mihimili ya uislamu ni undugu bila kubagua watu kwa misingi ya rangi, kabila, itikadi, na kadhalika.

Busaidy (1977), anapodai kuwa Mwenyezi Mungu ametuambia, "*Waislamu wote ni Hakika si jambo jingine, ni ndugu.*"

Mitazamo hii ni ya kina na kielelezo kwa kila adinasi. Wema unaweza patikana endapo watu wataghadhabiana na kutengana, basi amani itaonekana kwa wale wanaojamiana na dunia iwe ya kutamanika.

## 3.2 MISINGI YA TALAKA KWA MUJIBU WA UISLAMU

Kuna mikondo ambayo talaka hupitia kwa mjibu wa sheria na kaida za dini ya Kiislamu. Mwanamke ana wajibu wa kudai talaka kwa bwanake.

Mume ndiye wa pekee anayeweza kumpa mkewe talaka kwa mjibu na sheria za Kiislamu.Mwanamke ana haki ya kuidai talaka lakini anayetimiza na kuamua ni kwa njia ipi talaka hiyo inafaa ni mumewe. *Qur'an Tukufu* inasema kuwa*"Mwanamke yeyote anayemtaka mumewe talaka bila sababu basi ajue hataisikia harufu ya peponi hatauona ufalme wa milele."* (Sura ya 65:10)

Kila mwanamke wa kiislamu hutamani kutokuwa na visingiti vitakavyofungia kukosa kuingia Ahera au peponi.

Mulokozi (1975:46) anasema kuwa mwenye kufaa kutoa talaka ni mme wa mwanamke, na wala sio baba au kakake mume. Sharti awe na akili timamu, na iwe kwa hiari yake mwenyewe.

### 3.3 MISINGI NA SABABU YA TALAKA

Kulingana na dini ya Uislamu talaka ndio suluhisho la mwisho la kuachana kwa mume na mke kwa sheria na desturi za waislamu.Pande zote za mme na mke hupewa zi nafasi ya kuafikiana baada ya zogo na labda kurudiana baada ya masikizano mwafaka. El-Busaidy (1977) anasema kuwa kuna aina nne kuu za talaka. Nazo ni:

(i) Wajibu

(ii) Mustahili

(iii) Haramu

(iv) Makruhu

**Wajibu** ni talaka ambayo mme na mke hawapatani kabisa. Wao huwajibika kutafuta hakimu wawili mmoja wa upande wa mme pia wa mke na kuwahukumu kuwa mke atengane na mumewe.(apewe talaka).

**Mustahili** ni wakati ambapo mume anashindwa kumkidhi mkewe kwa mahitaji ya kimsingi kama vile chakula, nguo, au pesa za kujikidhi mwenyewe katika mahitaji yake.

**Haramu** ni talaka ambayo haifai kwa mjibu wa dini ya Kiislamu. Kwa mfano mwanamke anapokuwa katika hedhi huwa haina maana kwani ni jambo lisiloweza epukika na tena ni ya kiwakati.

**Mukruhu** ni msingi wa talaka itokeayo bila sababu yoyote. Endapo kosa ni la kwanza halistahili kuwa kizingizio cha kutaliki mwenzako kwani kisa cha kwanza halimwachishi mke.

Shabbir Ahmed (1998) anasema kuwa kuna aina *tatu* kuu za talaka.

*Talaaqe Rajee (Rejea) taalaaqe Mughallaza) na*

*Talaaqe baa-in (Bain)*

*Talaaque Rajee (Rajea*).

Talaka ya kwanza ya *rejea* ina mihimili inayosema kuwa bwana ampe bibiye talaka, na ilhali bibiye anaweza mrejelea bwanake baada ya makubaliano, mradi amrejelee kabla ya *Eda tatu* kuisha.

Tukifanya hesabu ya Tarikhi eda hizi tatu huchukuwa mda wa miezi mitatu baada ya kumpa talaka. Walakini baada ya kumrudia huwa hamna haja ya kufanya ndoa tena. Eda ni maana ya k*utambali* au kuzuiliwa na sheria kuingiliwa na mwanamme kabla ya mda wake kuisha kwa mjibu na sheria za dini ya kiislamu.

***Talaaque baa-in*** *(Bain*) ni talaka inayoachishwa na mme au mke mwanzoni mwa ndoa. Baada ya talaka *bain* kukubaliwa na pande zote mbili za mme na mke huwa ni nafasi ya sheria za ndoa na talaka kuachishwa na mke hawezi kumwita bwanake tena mpaka kipindi kilichowekwa kiishe. Endapo kipindi cha *Eda* kilichowekwa kuisha bila wao kupatana basi hawawezi kukubaliwa tena warudiane kwa mjibu wa sheria za dini ya Kiislamu.

Bwana na bibi wana hiari ya kuoa baada ya kipindi ambacho kimekubalika na mhujumu wa nikahi hiyo.

***Talaaqe Mughallazah*** ni talaka ambayo tunaweza iita ya ***kiupeo*** au ya mwisho. Talaka hii ndiyo ya mwisho pale ambapo mwanamme hana nafasi tena ya kumwoa tena au kurundiana na mkewe. Baada ya *Eda* kuisha mwanamke ana hiari ya kuolewa tena.. Endapo bwana atamtaliki bibiye, bibi huyo bado ana nafasi nyingine ya kumrudia bwanake wa zamani, endapo hapo mbeleni alikuwa ametalikiwa kwingine.

Jambo la kimsingi ambalo linajitokeza katika suala hili la talaka ni kuwa; talaka hata kama inaonekana ni ya haraka kwa mjibu wa sheria za dini ya kiislamu huchukua mda mrefu kabla ya hukumu la mwisho la kuachana kuafikiana. Ugomvi kati ya bibi na bwana kwa sababu *ya daawa (Kesi inayongojea uamuzi)* sii jambo linaloweza kusababisha ugomvi na fitina miongoni mwao kwani haikati kesi ya talaka moja kwa moja.

Ni wazi kuwa hakuna mwanadamu anayefurahia talaka kwani ndoa imeasisiwa kuwa ya kudumu ila kifo ndicho kinachoweza kuwatenganisha bibi na bwana.

Huku nikinukuu mwanamziki wa Kenya aitwaye Tony Nyandundo kwenye kanda yake iitwayo *Kidi Oba Etoke, Isanda gi Hera* (*Ndoa ya Machozi) VOL.1* ana wimbo mmoja unaoitwa *ndoa ya machozi.* Mwimbaji huyu anatoa taswira ya jinsi *talaka* huwa baada ya mme na mke kutalikiana. Mtunzi huyu maarufu wa midundo ya *Ohang'la* anafasili kuwa "*Ndoa ya mapenzi ikivunjika* huwa *ina machungu na mateso mengi sana*". Tunaweza kuafikiana na mwanamziki huyu kwa kiasi kikubwa kwani talaka ni chanzo cha shida ya waliopendana na kujuliana hali hapo awali.

### 3.4 UADILIFU KWENYE TUNGO ZA KITENDI

*Tendi* na mashairi katika diwani nyingi zinadhamiria kuakisi umuhimu wa kuadilika miongoni mwa jamii, kwani mashairi yalitumiwa na watunzi si kwa kuwachangamsha wanajamii bali jamii ilipewa maarifa na ushauri wa kimaisha kupitia sanaa kama hizi. Mungania (1985:35) anasema kuwa maadili ni mafundisho yatolewayo kwa njia ya ushairi na ambayo huongoza kwenye haki. Hakuna jambo lililo mbaya zaidi kuliko kupotea kwa utu wake.

Fafanuzi hizi zinatupa uelekezi wa jumla kwamba tungo zinawajibika kuongoza na kuipa jamii mkondo mahsusi wa kiuelekezi na hasa utu na tabia ya kutamaniwa na kila adinasi. Sanaa ni *gari* la kuelekeza jamii kwa uwanja wa wema na uajibikaji wa nyendo nzuri na kuasi maovu yanayopotosha jamii. Mtunzi mwingine mwenye umaarufu kwa diwani zake za kimaadili ni Amir (1959).

Mtunzi huyu amelenga na kutambua jamii zinazoshuhudia maovi wakati wa enzi ya ukoloni wa Wajerumani na Waarabu nchini Tanganyika kama ilivyokuwa vile Tanzania ilivyokuwa ikiitwa hapo awali. Mtunzi kwa kupitia tungo zake mwanzoni za mwa mwaka wa (1957-1959). Ametunga tungo za kimaadili kama vile *Uhuru wa Tanganyika.* Mtunzi anatoa picha ya kisaikolojia ya jinsi Waarabu walivyokuwa walaghai kwa kuwadhulumu wananchi wenzao kwa kuwafanya watumwa, kuwatumia vibaya na kuwauza ugenini.

Mtunzi anatoa taswira ya watu wasiokuwa na uadilifu na utu kwa jamii nyingi za Kiafrika. Yeye ametuteka nyara kwa kubuni matukio yenye hisia za kulipiza kizazi. Waarabu nyakati za zamani walifanya biashara ya utumwa, hivyo basi waliweza kunufaika ilhali wenyeji wakaadhabika kwa mateso kwa biashara zao zilizokiuka kaida za kiutu. Mtunzi anasema: (Ub.39)

***Hebu nanyi jaribuni***

***Muyatie akilini,***

***Hivyo ni kufuru gani***

***Mwenzio kumtendea***

***Kulipa pembe makamu***

***Kuliko ya binadamu***

***Asichelee jukumu***

***Kwa tama ya rupia***

***Wenye mimba matumboni***

***Wakazalia porini***

***Kwa mikwaju maungoni***

***Na twika zawangojea.***

Mafunzo yanayojiakisi kwenye ubeti huu yana dhana ya kutoadilika. Mihimili moja mikuu ya dhana ya uadilifu ni kuwa na utu kwa mwenzako katika jamii inayodumisha utamaduni wa kuaminiana na kuboresha maisha kwa pamoja bila chuki wala ghadhabu.

Sanaa ina jukumu la kufichua ulaghai unaoakisi jamii hata kama itambidi mtunzi amulike viongozi bila kubagua kwani mwandilifu huwa na moyo mkunjufu na hujiepusha na kupaswa kuishi maisha mema ya ktamaniwa na wanajamii popote atakapoishi.

## 3.5 DHANA YA TASWIRA

Fasili ya taswira imethibitiwa na wahakiki wengi wa kifasihi kwa njia tofauti. Kahigi (1979:28) anasema kuwa taswira ni matumizi ya lugha yanayo pambanuliwa na utunzi mzuri wa maneno, uangalifu na udhahiri wa maelezo, wenye kuhusisha na kujumuisha dhana mbalimbali tofauti ndani ya dhana moja; ili kuleta athari maalum katika mawazo ya msomaji au msikizi.

Kwenye maelezo ya mhakiki huyu tuna msingi wa istilahi hii kwa kutazamia kuwa kuwa taswira huleta athari fulani katika uamuzi wa mtu kuhusiana na matini anayoisoma au kukumbana nayo. Taswira ni kigezo ambacho kina nguvu zake ambazo zimfanya mtu kuelewa yale ambayo anakumbana nayo, iwe ni matini au

ujmbe kwa njia ya maongeo kwa upande mwingine ina *kawi* maalum kwa msomaji au msikizi.

Senkoro (1982:36) anawaza kuwa "taswira ni *lugha ya picha.* Picha hizi huweza kuwa za wazo, kitu, hali, dhana au uzoefu fulani katika jamii'.mwanafasihi huyu aliibua aina tatu za taswira kama vile ;Taswira zionekanazo, taswira za mawazo,naTaswira za hisi .

Kulingana na mhakiki huyu taswira ni picha zinazoundwa akilini mwa mtu na ambazo zina mguzo na matendo yanayooeza kuonekana kama vile sogora anaye kupiga ngoma.

Mulokozi (1999)anadai kuwa taswira ya kimawazo ni taswira ambayo ni kidhahania.Hukuzwa akilini mwa wanadamu kwa njia ya kisaikolojia na ya kuwazika tuu.Kwa mfano kuwaza Moto wa jahanamu ni jambo la kuwaza na wala sio jambo ambalo linaweza kuonekana.

Taswira ya hisi hutumika kwa kuhusisha hisia zote tano za mwanadamu. Nazo *ni kunusa, kuonja, kusikia, kugusa, na kuona.*

Kulingana na maelezo ya mhakiki huyu kuna udondoshi ambao tunaweza kuutoa kuhusu fasili yake kuhusu taswira. Taswira ni wazo ambalo hujengeka akilini mwa mtu anapowazia jambo fulani. Pili mawazo hayo ni ya kisaikolojia na hujengeka kwa misingi ya tajriba ya yule anayewazia.

Welleck na Wellen (1982:189) anasema kuwa taswira ni chochote kile kinachofanana na kitu au jambo Fulani, picha ya kimawazo, au kiwakilishi bayana,

Maoni ya wanafasihi hao wawili yanatuelekeza kujumlisha uhusiano ulioko kati ya taswira inayokuzwa akilini kama mawazo na ishara za kuonekana zinazoachilia wazo Fulani lililobuniwa akilini.

Msokile (1993:45) anawazia kuwa taswira ni zao la fikra na hujengwa kutokana na matumizi ya tamathari za usemi hasa sitiari na ishara mbalimbali zenye kuhusu mawazo, dhana, vitu au maumbile.Msokile anawazia kuwa mihimili ya taswira ni matumizi ya tamathari za usemi huku akitilia maanani sitiari na istiara.

Kwa upande mmoja tunaweza kukubaliana naye na kwa upande mwingine tunawaza vingine.Mwanzo kabisa tunastahili kujiuliza swali hili. Jee mtunzi akitumia mbinu zingine zozote na picha ya kimawazo ionekane hatakuwa amefaulu kuonyesha mawazo yake ya kisaikolojia? Kwa maoni yetu sio lazima tamathari za semi zisheheni taswira ya kimaandishi bali ni uteuzi wa msamiati na ubunifu wa lugha utakaibua taswira yenye kunata hisia za msomaji au msikizi.

Knappert (1979; 70-71) kwenye *Wimbo za Fumo Liyongo* uitwao *Wimbo wa nyika* mtunzi anafanikiwa kuonyesha pisha halisi ya makazi ya Fumo Liyongo kwa kupamba lugha yake ya wimbo huu anaposema;

***Mwana wangu nakusimulia***

***Ya Liongo Fumo wa vishaka***

***Hana kufu, huishi huria***

***WamfanyaFumo wa Wanyika***

***Hali wali, havaihariri***

***Hula wimbi na nyama ya mwituni***

***Huikata na yake hajali***

***Wala hali masazo ya watu.***

Tunapowazia ubeti huu unaotolewa kwenye nyimbo zake za jagina za Waswahili tunapata picha kamili ya kule alikoishi bila kuzingatia tamathari za semi.Tunyaona akilini mwetu mazingira yale aliyokuwa akiishi kama vile nyikani na mwituni, na pia na kugundua kuwa aliishi pekee.

Coombes (1953:52) anaelezea kuwa mwandishi mzuri hufanikiwa wakati anapotumia taswira kwa *ulegevu.* Ukwasi wake katika kufahamu na kujali kwake katika kueleza *anayohisi* kumsaidia kuumpa picha ambazo zina uhusiano wa moja kwa moja na yale anayohisi.

Mkabala huu wa Coombes unatuelekeza kwenye swali letu la utafiti. Taswira ikitumiwa kwa ulegevu inaweza changia kuvuta hisi za msomi. Haya ndio maswali ambayo tunawazia kuyajibu kwenye utafiti wetu.

Kahigi na Mulokozi (1979;28) wanasema kuwa taswira ni picha ya matumizi ya lugha yanayo pambanuliwa kwa utunzi wa maneno kwa uangalifu na udhahiri wa maelezo wenye kuhusisha na kujumuisha dhana moja ili kuleta athari maalum katika mawazo ya msomaji au msikilizaji .

Maoni ya wahakiki hawa ni ya wazi kuwa athari fulani huakisiwa baada ya kuleta udhahiri wa maelezo unaoungamanisha mawazo ya kimseto yanakuzwa akilini na kuleta wazo mpya akilini.

Njogu na Chimerah (1999;91) wanaelezea kuwa taswira hutumika kuleta picha au hali fulani akilini mwa msomaji au mtazamaji. Anaweza kuona, kunusa, kuonja, kusikia, au kudharau kilichosawiriwa kutegemea nguvu za taswira zilizotumika.

Wahakiki hawa wameangazia dhana ya hisia za mwanadamu kuweko kwa taswira zinazoasisiwa.Kwa maoni yetu tunaweza kukubaliana na wahakiki hawa kwa upana

kwani mtunzi akiwazia hadhira yake ilie, icheke, isikize ujumbe na hata kuonja hayo yote yanaweza kufungamanishwa na uangavu wa taswira.

Wamitila (2003:225) anafasili kuwa taswira ni dhana inayotumiwa kuelezea neno,kirai au maelezo ambayo yanaunda picha fulani katika akili ya msomaji. Taswira zinaweza kuwa za kimaelezo au Kiishara ishara ambazo zinaunda picha fulani au imeficha ujumbe mwingine. Dhana ya taswira ni pana na wala sio tu uamilifu wa kipengele hiki kama tamathali bali ni kipengee kipana kwa utendakazi wake.

## 3.6 HITIMISHO

Kulingana na maelezo ya wahakiki wale wote ambao walitoa fafanuzi mbalimbali kuhusu taswira, imedhihirika kuwa taswira hujengeka wakati mtunzi anapounda maneno na kuwazia wazo la kisaikolojia. Kwa maoni yetu matumizi ya tamathari za usemi ni mojawapo wa visaidizi vya kuundia taswira na wala sio kaida ya kufuatwa kwa lazima ili kigezo cha taswira kiafikiane. Kinachotokea muhimu ili taswira inate akilini mwa msomaji ni jinsi lugha inavyofinyangwa ili kuleta athari fulani akilini mwa msomaji au msikizi.

## SURA YA NNE

### 4.0 UTANGULIZI

Sehemu hii ya uhakiki wetu ndio inakusudiwa kuwa upeo wa utafiti wetu. Tunadhamiria kuchanganua dhima ya kipengele cha maudhui.Bali na hayo azimio la kudhinisha kana kwamba kuna uvuto wa kipekee unaojisheheni kwenye kipengele matumizi ya taswira kama mbinu mojawapo ya mtunzi.

Ni katika sura hii tutakapodadisi mifano mahsusi ya maudhui ambayo imeibuka kwa sababu ya matumizi ya taswira kwa *ulegevu?*

Knappert (1967:7) anadai kuwa *Tendi* zilitungwa kwa minajili ya mafunzo au uelekezi maalum wa kina. Aidha tutadadisi mafunzo muhimu yanayojitokeza kwenye utendi tunaouhakiki.

### 4.1 ASILI YA UTENDI WA SIIRAJI

*Utendi* wa *Siiraji* una umaarufu wake kwani umo kwenye maktaba ya Uingereza ijulikanayo kama *School of African Studies (S.O.A.S)* na umehifadhiwa kama mswada (Na. 380761, MK 380066). Kulingana na rekodi ilioko kwenye maktaba hiyo ya Uingereza, *Utendi* huu ulitungwa mwaka wa 1346AH/1927 ***BK*** na Muhammadi Kijumwa kwa lahaja ya kiamu. utendi huu una beti 209.

Abou, Egl (1983) anasema kuwa yeye ndiye aliyeunakili kutoka kwa hati ya Kirumi hadi Kiingereza. Dhamira na kusudio la mtunzi wa utendi huu ilikuwa kumwusia mwanawe wa kipekee wa kiume Bwana Helewa. Mtunzi amenuia kumpa mwanawe mawaidha ambayo angeyatumia ili asipotoke na kukosa mwelekeo wa kimaisha.

*Utendi* wenyewe unaitwa "*Siiraji*" maana yake ni"*taa*" ishara ya mwangaza kama nilivyokuwa nimetaja hapo awali. Kulingana na mtunzi umetungwa kwa kulenga

vijana ili waadilike maishani mwao ya siku za usoni.kuachilia mwanga utakaomwelekeza mlengwa kwenye fadhili za maisha mema.

Abou Egl (1983) anafafanua kuwa *utendi* huu unatupa picha

Ni bayana kuwa mtunzi amelenga kumuusia mwanawe aliyekuwa ametorokea Unguja baada ya kukosa na babake .Ub.6 unadadisi hayo.Helewa alikuwa mwanawe wa kiume wa kipekee aliyezaliwa mwaka wa 1892. Mamake aliyeitwa Fatuma bin Mataka alikuwa mkewe wa pili wa mtunzi.

Ni wazi kuwa Helewa aliaga mwaka wa 1958 huko Mombasa akiwa na miaka 66 na ni ukweli mtupu kuwa alikuwa ametoroka nyumbani na kuishi ugenini kwa mda mrefu na kufanya kazi hii iwe na uhalisia wa kipekee. Ub wa 206 unadhibitisha ya kuwa walikuwa wamekaa kwa mda bila kujuliana hali anaposema;

***Siku nyingi sikuoni***

***Sute hatudirikani***

***Ndipo name katamani***

***Kama haya kukwambia***

Aidha mtunzi aamelenga utungo wake uwafaidi wajukuu wake , kwani alihofia angeaga dunia bila kumwona mwanawe wa kipekee , Kama ilivyokuwa desturi ya Waswahili kuwausia wana wao. Ubeti wa 206 una kauli hilo la kuusia hata nasaba ya mtunzi anaposema;

***Mushike wasia wangu***

***Nimewambia wanangu***

***Tawabirikia Mungu***

***Hini dira safari.***

## 4.2 DHANA YA MAUDHUI

Ni kweli kuwa msanii huwa na uhuru mkubwa wa kuteua lugha, mada na ujumbe anaoukusudia uwafikie hadhira yake.

Msokile (1993:58) anasema kuwa maudhui ni jumla ya mambo yanayoelezewa ama kujitokeza katika kazi ya kifasihi .Maudhui ya kazi ya kifasihi hujumuisha dhamira, mtazamo ama msimamo, ujumbe, maadili na falsafa.Mawazo ya mhakiki huyu yameonyesha uhusiano sawia dhamira na ujumbe unaokusudiwa kuwasilishwa na mtunzi kwa njia .ya kimaandishi.

Mungania (1985) anasema kuwa mwandishi huandika yale ametayarisha kuwasilisha kwa njia ya ubunifu .Hapo ndipo mhakiki anapofasiria msomaji ili aone mambo kwa uwazi na kwa kupenya jicho la ndani kuliko alivyosoma awali.

Kwa msingi huo tuna azimio la kuchanganua aina mbalimbali za maudhui na jinsi kipengele cha taswira kinavyotenda kazi ili maudhui ya mtunzi na yatakayotokana na utafiti wetu yaaangaziwe.

## 4.3 MAUDHUI YA *UTENDI* NA TASWIRA HUSIKA

Katika awamu hii tutachanganua aina mbalimbali ya maudhui na kuonyesha jinsi mtunzi amepenyeza mbinu ya taswira ili maudhui yake iwe na dhima .Jee ni katika uwasilishaji wa picha zinazoundwa kwenye akili hufanikisha maudhui ?

.Maudhui yanayotokea ni ; tamaa na uhoro, umakini, ukarimu, tabia njema, ndoa, ufaragha/usiri, suluhisho na mapatano, bidii, imani, na wema na utu,usikivu na uelewaji, utiifu, na haki.

### 4.3.1 TAMAA NA UHORO

Mtunzi anamkanya mwanawe asiagize zaidi ya kipimo cha matumizi yake .Amepewa mifano mibaya ya tamaa kwa kuonyesha picha humhusumtu mwenye sifa na ishara za tamaa kama vile *kurambia vidole kwenye sinia* ,na kuonyesha uhoro wa hali ya juu. Sio tu tamaa ya kutaka kula chakula kingi kuliko kipimo cha uwezo wa mtu wa chakula bali tamaa ya kutaka kumiliki mali isiyo halali . Ubeti. wa 137 unayadhihirisha hayo anaposema ; Mtunzi anasema;

***Na kuteua zinofu***
***Ambazo zilo nadhifu***
***Ili ruhu kuidhifu***
***Aibu hukuvutia***

Taswira anayopenyezwa na mtunzi ni hisia za kuonekana .Tunahisi kana kwamba tunamwona mhusika huyu wa kimawazo akifanya vitendo hivyo tulivyovitaja vinavyodhihirisha tamaa na uhoro ambayo kweli ni tabia hasi. Tabia io hiyo imewasilishwa kwenye Ubeti wa 135 wakati mtunzi anaposema aasi tabia ya kula upesiupesi kwani huenda akanyongwa na chakula hasa vidonge vya nyama na labda kuaga au kuaibika mbele ya watu huku anasema;

***Kula upesi upesi***
***Fanya mambo kwa kiasi***
***Mara zitakupalia**Ub.137*

### 4.3.2 UMAKINI

Maudhui ya umakinifu imeangaziwa kwa wingi. Umakinifu kwa maoni yetu ni hali ya kuwa muangalifu kwa jambo lolote mtu afanyalo.Maudhui haya yamebuniwa katika ubeti wa 182 ambapo mtunzi anasimulia jinsi kipepeo anavyojitoza kwenye moto kwa kutokuwa makini kwa ya anayoyafanya.Anaombwa asisuhubiane na marafiki wabaya watakaomwingiza kwa mitego ambayo itakuwa shida kujitoza na kujinusuru.

Ni kweli kusema amewasilisha picha ya mdudu huyo, ili maudhui yake yaeleweke kwa kina na kwa njia iliyo makinifu na ya kuaziwa kisaikolojia na mtu atayepata nafasi ya kudurusu utenzi huu .Ubeti wa 182 unasema;

*Usiiweke matandi*
*Baba angalia pandi*
*Kwenda taani hatindi*
*Hata akateketea.*

Mtunzi anasisitiza thamani ya uhusiano mwema kwa makini kwa wale anayesuhubiana nao .Ni vyema kuchagua masahibu wenye maadili mema kwani wengine hutubukuza wenzao kwenye mabaya kimaksudi na kuwacheka baadaye wasijue jinsi ya kujinusuru kutoka kwenye shida .

### 4.3.3 UHUSIANO NA USHIRIKIANO

Kwa maoni yetu uhusiano ni hali na jinsi mtu hushikilia mtu mwingine kwa hali na mali.Aidha ushirikiano ni kufanya kazi pamoja .Mazrui(1992)anasema kuwa

ushirikiano una sifa za uhusiano.Hivyo ni kusema ya kwamba hakuna mpaka kati ya uhusiano na ushirikiano.

Mtunzi anamshauri mwanawe awajibike kwa kuwa kielelezo kizuri kwa jamii yake sio tu machinani, bali aidha anapoenda ng'ambo. Ubeti wa 117 unayasimulia hayo;

***Ukiwako ugenini***
***Ukamwona mwendani***
***Wa ishifaki amini***
***Shauri naliwe moya.***

Picha anayoachilia mtunzi ni picha ya kimawazo inayokuzwa akilini mwetu na kutaka kuiga tabia hiyo bila kushurutishwa na mtu yeyote.

### 4.3.4 UKARIMU

Ukarimu ni kinyume cha mtu kuwa na sifa za uchoyo. Kamusi ya Tuki (2008) inafasili ukarimu kama kitendo cha kuwapa watu vitu vya kimahitaji. Ukarimu ni hali ya kusaidia wenye kuhitaji msaada kwa hiari za mtu binafsi bila kushurutishwa na mtu yeyote.

Mtunzi amebuni mawazo yanasawiri vitendo vya ukarimu kwani ukarimu ni jambo la kidhahania. Mtunzi amesisitiza ukarimu umiminiwe kwa marafiki, majirani, wagonjwa, na watu wote wasiobahatika kenye jamii.

Mwandishi amemsihi mwanawe Helewa awatunukie misaada watu wanaohitaji bila ubaguzi kwa kutenda haya itakuwa ishara ya ukarimu. Kitendo cha kupeana ni mojawapo ya *nguzo* tano za *Uislamu* ambacho ni *zaka* au *Zakat.*

Mtunzi anaeleza jinsi mtu anaelezea jinsi ukarimu unavyoweza kutunukiwa wasiobahatika kama vile, nguo, mikopo hata mikopo ya pesa. Ubeti wa 23 unayakisi hayo anaposema;

***Mwendo kikuhitajia***
***Bure karidha akiya***
***Mapesa nguo rupia***
***Ulichonacho ridhia***

Taswira inayopenyezwa kwenye maudhui haya ni taswira ya mguso.Taswira ya mguso ni taswira yenye vitendo vinavyoonekana bila kuwazia moja kwa moja. Kitendo cha kupeana bidhaa za kutumia kama vile pesa, na nguo ni vitu vinavyoweza kuonekana ingawa ni kwa njia ya kuwazia.

### 4.3.5 WEMA NA UTU

Kulingana na Kamusi ya karne 21, Ni mambo mazuri anayoyafanya mtu, jamala ya kuenziwa.. Kutokana na fafanuzi hizi tunaelewa kuwa wema ni jambo au kitendo cha mambo mazuri.

Kwa maoni yetu utu ni hali ya kuwa na sifa njema kwani ni vitendo vinavyotoa sifa nzuri za kiutu. Ni tendo la ubinadamu kinyume na uhayawani.Wema ni hali ya kuwa na uzuri na matendo yanayokubalika na mbeko za jamii husika.

Msimulizi amehimiza mwanawe awe akimpa mkono wa kheri wale watu wasio bahatika kama walemavu, maskini, wagonjwa, hata wale *waliojaa vidonda mwilini.*

Mtunzi ananukuu wema na utu wa Mamake Kamari nyanyake Helewa kwa jinsi alivyowatambua wasiobahatika kwa kuwapa misaada ,bila kuchoka wala kuonyesha ubaguzi wala mapendeleo.Ubeti wa 75 unaelezea ;

***Kwa mamangu walikiya***

***Magonjwa yamewenea***

***Sikuona siku moya***

***Pua akiwashikia.***

Ubeti huu unaelezea jinsi kijana Helewa hastahili *kushika pua* endapo wagonjwa wanaobisha hodi kwake kutaka msaada kwa vidonda vya mwili, bali awape mkono wa kheri kama ilivyo desturi ya ukoo wao.Aidha ubeti wa 73 anayakisi ambayo tumetaja;

***Tongo kiguu akiya***

***Na gonjo limwenea***

***Mlango kakugongea***

***Chochote humwatia.***

Taswira ambayo inayoachiliwa inayoingiliana na maudhui haya ni ya hisi za kunusa. Msimulizi ameangazia jinsi wagonjwa wenye vidonda wanavyotoa uvundo kuachilia tuhisi kushika pua hata kama ni kwa kuwazia tu.

### 4.3.6 TABIA YA WAKATI WA MAANKULI

Tabia ni matendo ya kimazoea ambayo mtu husifika nayo. Kamusi ya karne ya 21 (2010) inafasili ni matendo ambayo mtu amezoea kuyafanya mara kwa mara na kwa udesturi". Maudhui ya ushukulio wa mtu wakati wa maakuli umesheheni pakubwa .

Ni vizuri kutambua kati ya ubeti wa 128-166 umeangazia tabia ya mtu wakati wa mankuli . Beti 38 zimesawiri tabia ya mtu wakati wa mankuli. Ni desturi ya Waswahili kukulia kwenye sinia moja wakiwa pamoja.Ubeti wa (134) unawazia jinsi mhusika huramba vidole kwenye sinia huku akikosa kutambua hisi za wale wanaokula nao kwa pamoja anposema;

***Na kufuta ukungoni***

***Kwa mkono sahanini***

***Zanda kutia kanwani***

***Haya huyashinda pia (Ub 134)***

Mtunzi anatushirikisha kwenye hisia za uojo. Kwa upande mwingine taswira ambayo mtunzi ameangazia inamfanya msomaji kupatwa *na kinyaa* cha baada ya kudurusu sehemu hizi .Aidha tabia hii tunaihisi moja kwa moja hata kama ni kwa njia ya kuwazia.

### 4.3.7 UTOVU WA NIDHAMU

Ufafanuzi wetu wetu utovu wa nidhamu hauwezi ukafasilia kwa njia ingine ila kusema kuwa ni hali ya kuegemea kinyume na matarajio ya mbeko na tamaduni za jamii husika kwa maoni yetu. Dhima hii inahusisha tabia na mtu binafsi na ushukulio wake na wanajamii wanaoishi pamoja.

.Mtunzi anasheheni utovu wa nidhamu anapoangazia jinsi anavyostahili kufanya endapo anahisi kutoa makamasi kwa pua asipanguzie kwenye ukuta badala ya kwenye nyayo zake.Ni wazi kuwa jambo kama hilo ingeleta mushki miongoni mwa watu endapo tabia kama hiyo ingemsheheni.

*Kwamba ukuta huoni*

*Kheri futia guuni na koo hadhirani*

*Na koo hadhirani*

*Enda nde kufutia (.Ub.107)*

Walakini mtunzi amekulia kwenye enzi ya utamaduni wa Kiafrika na vitambaa vya makamasi vilikuwa nadra? Picha ya mawazo tayari imekuzwa na mtunzi kufanikiwa kuwasilisha maudhui yake.

**4.3.8 SULUHISHO NA MAPATANO**

Mtunzi amesisitiza mwanawe mfano mwema wa msuluhishi na mpatanishi wa watu wanaozozana. Mwandishi anamshauri asiwaache marafiki wake wakizoza na kupigana, bali awe mpatanishi wa kweli.Aidha ameshauriwa awe mtenda haki na hakimu wa ukweli.

Ubeti wa 19 na 20 unayadhibiti hayo;

*Na mwendo ukimkuta*

*Yeye na mtu huteta*

*Siwapendelee zita*

*Amua ukyangukia (Ub.19)*

*Mwendo mukifuatana*

*Kaya mtu wakawana*

*Kitangiliwa si sana*

*Sishawiri nawe ngia (Ub.20)*

Mtunzi anaelekeza fikra zetu kwa mazingira ambayo kitendo hicho cha vurugu hasa cha vita hasa kati ya marafiki wawili yanatendeka.Tunawaza kitendo cha watu wawili

Aidha ni katika ubeti wa 170 mwandishi anawaza ingefaa atafute mchumba wa daraja lake kiuchumi .Jee, ni vyema kuiga ushauri kama huo?Labda ni jambo ambalo linaweza kuwa na mjadala.Msanii anasema;

*Zegea mwana wa*

*Kwako*

*Au wa daraja yako*

*Lisitawi ina lako*

*Na wenye kukwangalia*

Kwenye Ubeti huu wa 171 babake anasisitiza mhusika awe akimfurahisha mkewe kwa hata kurejelea nyumbani mapema na kuepukana na vurugu za kinyumbani anasema;

*Mke wako mpumbaze*

*Kwa uwezalo mweneze*

*Na wewe simteleze*

*Nde ukalimatia (Ub.171)*

Misululu ya picha tunayoizua akilini mwetu ni ya kuwazia jinsi ndoa ya kutamanika inavyostahili .Ni wazi kuwa mapenzi hayawezi yakatazamwa kwa macho bali vitendo vinaweza akidhi mapenzi ndoa safi.

### 4.3.10 UTIIFU

Ni katika kwenye mawazo yetu tunapofasili dhana ya utiifu kama hali ya kufuata sheria na kaida ambazo zimeteuliwa na kikundi fulani cha jamii ili kuboresha maisha ya kila mtu.. Ni hali ya kutekeleza wajibu wa mbeko fulani. Mtunzi amepeana mfano mzuri wa kutii wazazi.

Mwandishi anahimiza umuhimu wa kuwatii hata wazazi. Katika ubeti 84 msanii anahimiza heshima ya mzazi ipewe kipao mbele anaposema ;

***Mtii baba na mama***
***Hata wakikusukuma***
***Inyamaze yatakoma***
***Simjibu ovu moya(Ub.84)***

Katika *Biblia Takatifu* kuna amiri kumi za Mungu. Amri ya nne inasema tutii wazazi wetu ili siku zetu za duniani ziongezeke.

Wazo hili la utiifu na kuaminika miongoni mwa jamii ujitokeza pale ambapo mtunzi anatoa wasia wake kwa mwanawe kwa kumshauri asidhubutu kuwa na mienendo ya kupekuwapekuwa daftari,barua na vitabu vya wenyewe bila idhini ya mwenyewe anaposema;

***Mtu ukingia***
***Chuo dafutari pia***
***Si haja kumsomea***
***Na barua zote pia.***

**4.4 MAFUNZO MUHIMU**

Kwa kutambua mafunzo yanayotokana na udurusu wa utendi huu tutakuwa tumefaidika kwani licha ya kuchanganua maudhui tumewadia kuangaza mafunzo muhimu tunayoyapata kwenye utungo huu.

### 4.4.1 UTAMADUNI

Ni dhahiri kusema kuwa hata kama Waswahili waliiga Waarabu tabia za maisha yao, bado wengi wa watafiti wa enzi hizo kama vile Kijumwa hawakukengeushwa na tamaduni za kigeni. Wafrika walihifadhi mila na desturi zao zilizoridhiwa na kizazi kimoja hadi kingine.

Hichens(1972) anasema kuwa Waswahili walioishi upwa wa pwani ya Afrika Mashariki walikuza na kuhifadhi utamaduni, mila na mbeko zao kwenye fasihi simulizi na baadaye andishi kwa *nyimbo, Tendi, mashairi, na mitindo* yao ya kufanya kazi.

### 4.4.2 MALEZI BORA YA WATOTO

Mtunzi amesisitiza kuwa pana haja ya kulea watoto bila kuwadekeza. Jukumu la mzazi ni kuwapa watoto mahitaji yao ya kimsingi na pia kuwashauri na kuwaelekeza endapo wataiga tabia mbaya maishani mwao.Ni jukumu la kila mzazi au mlezi kuwaelekeza na kuwashauri watoto kwa manufaa yao na kwa nchi kwa ujumla. Katika *ubeti* wa 47 mtunzi anisisitiza wanafunzi waachishwe tabia ya kuobaoba nyumba kwa nyumba bidhaa za kuwakidhi maishani mwao.

Mtunzi anahimiza endapo kuna tabia hasi inayoigwa na mtoto ni jukumu la mzazi kuachisha tabia hasi na kuangaza tabia chanya.ubeti wa 47 anpolenga watoto wa shule;

***Wenu wana wa chuoni***

***Kapisa siwalicheni***

***Wakiomba majumba***

***Kuomba watazoea***

### 4.4.3 UVUMILIVU NA SUBIRA

Uvumilivu na subira ni hali ya kungojea jambo kwa njia ya matumaini. Uvumilivu ni mbinu ambayo inaweza kutupandisha binadamu kutoka daraja moja hadi nyingine.asiofikiria anawezafika.Uvumilivu kwa wakati mwingine huingiliana na dhiki. Maisha ni kupanda na kushuka. Mtunzi anasisitiza kuwa hata kama ni kufungwa jela kuweko na uvumilivu.

Ubeti wa 58 na 59 unayasi masuala ya subira na uvumilivu.

***Subiri subira njema***

***Sidumu na kulalama***

***Mwishowe huma malama***

***Ukilalama si dawa***

Ni vyema kuwa na uvumilivu hata kama maisha yanaonekana kuwa magumu kwani mvumilivu hula mbivu kama tunavyoweza kuichukulia funzo hili la uvumilivu.

### 4.4.4 USIKIVU NA UELEWAJI

Usikivu ni hali ya kutulia na kusikiza ujumbe unaowasilishwa na msemaji kwa njia mbalimbali za mawasiliano. Hisia zinazojidhihirisha katika kitendo hiki ni hisi za usikivu ambazo kudadisiwa na kiongo cha mwili cha kusikia cha masikio.Mwanadamu yeyote yule sharti atilie maanani mbinu ya usikivu la sivyo ujumbe utakosa mwelekeo.Endapo mtu hatashika kile ambacho ameelezewa huenda akasimbua ujumbe huo kinyume na matakwa ya mnenaji

Paul Grice (1975) anadai kuwa kwa kawaida binadamu hunena machache yenye kubeba maana zaidi.

Mbinu ya usikizi ni muhumu kwani ndio huzua umaanisho au uelewaji wa ujumbe na kuwa chanzo cha kusimbua ujumbe kwa inayofaa.

Mtunzi anahimiza dhana ya usikivu kama kigezo kikuu kinachochangia uelewaji wa ujumbe. Yeye anasisitiza msikilizaji aitenge wakati wa kusikiza ujumbe hata kama ni dakika tano Ub wa mstari wa tatuanasema;

***Mtu kikwambia neno***

***Sijibu upesi mno***

***Ingawa dakika tano***

***Kheri kwanda kusikia.***

Ni katika sehemu hii ambapo mtunzi anapohimiza usikivu wa kina ili uelewaji wa ujumbe na kujibu au kutekeza wajibu ufikiane kwa dhati. Mtunzi katika uliokusudiwa.

Maudhui haya ya usikivu na uelewaji wa ujumbe uaasisi taswira ya hisi hasaa ya usikivu. Utunzi unatilia mkazo dhana ya usikivu na uelewa ili kusimbua ujumbe au kutekeleza ijumbe ipasavyo.Hisia za usikivu hivyo basi ni muhimu na mtunzi ametuagiza kusikiza kwanza kabla ya kulitenda jambo. Taswira ya hisi huwa zina nguvu ya kuganda akilini na kunasisha ujumbe wa hadhira au wasomaji kwa ujumla.

### 4.4.5 IMANI

Kulingana na Kamusi sanifu (2004:120) Imani ni mambo anayokubali mtu kuwa ni ya kweli na anapaswa kuiheshimu hasa katika dini. Kulingana na fasili hii, imani ni jambo la hiari na linatokana na kushawishika kwa mtu binafsi.

Ili ayadhibiti yale anayoyaona kana kwamba ni ya ukweli.

Msisitizo mwingi wa imani ya dini ya Kiislamu umesheheni kwenye Utendi wenyewe. Imani ya dini ya kiislamu inahimiza udugu na mapenzi ya dhati, uaminifu

wa nguvu na uwezo wa mwenyezi Mungu ambao unakinga mja kupigana na mateso, na vishawishi vya dunia na kuchukua mkondo wa kheri na baraka. Imani ya dini ya Uislamu inaamini mafunzo ya kitabu kitakatifu cha *Qu'ran* kana dira ya uumini wa kila mfuasi wa dini hiyo

.

Mvumbi (2008:19) anasema kuwa umuhimu wa *Qur'an* umo katika asili yake maana na yaliyomo. Kwanza inatazamiwa kama kitabu cha Mungu, chanzo cha uislamu kwa kuwa humpa elimu ya msingi yeyote aliye na hamu ya kuelewa uislamu. Pili ni malighafi ya elimu ya kiislamu. Utendi tunaouhakiki unahimiza usomaji *wa Qu'ran Tukufu* na utekelezaji wa masomo hayo.Utendi huu umenukuu aya nyingi za *Qu'ran* huku mtunzi akiapa kuwa anaielewa *Qu'ran* tukufu kwa dhati. Nukuzi zingine ni za moja kwa moja kutoka kwa kitabu kitakatifu, wakati anposisitiza ushauri Fulani.
Mtunzi anamenga mashauri yake yaoane na imani na dini ya Kiislamu ili ushauri wake uchukuliwe nkwa hadhi zaidi. Kwenye aya ya 16 mtunzi ananukuu kuwajibika mwanawe kuwajibika na kuiga mafunzo ya *Qu'ran* na Allah na kumshauri kuwa endapo atachokozwa yeye ayapuuze mambo kama hayo kwani Mungu atamlipizia kizazi.

***Kuruani imenena***

***Nimesoma nawe ona***

***Andao shari ni sana***

***Kujibu alokwambia***

***UB.34***

Mtunzi katika UB.70 ameonyesha msingi wa imani ni kunyenyekea na kuomba msamaha kutoka kwa Mungu naye humkubali yule anayemrudia. UB. wa 70 unakiri hayo;

***Kurani hutwambia***

***Nawe soma hiyo aya***

***Tooba ukitubia***

***Toba Mungu hupokea***

Ni kwenye Ub.wa 70 ambapo mtunzi ananukuu *Qu'ran Tukufu* aya 27 ambayo inasema; "Na yeye anayekubali makosa yake na kukiri makosa yake husamehewa dhambi zake, anajua anachofanya."

**4.4.6 KUTENDA HAKI NA UKWELI**

Kutenda haki ni hali ya kukata ushauri au kesi, bila kuegemea upande wowote. Mtunzi anasisitiza ni wajibu wa kila mtu kumtendea haki, bila misukumo ya upendeleo Fulani wa mtu unayekusudia kutendea haki.

Mtunzi ameangazia dhana ya kutenda haki na ukweli katika ubeti wa 27. Utendi unahimiza ushahidi wa kweli na kukiuka uwongo mbele ya mahakama, iwe nduguyo wa tumbo moja, unayemtetea.

aNi wajibu wa kila mtu kumiliki ukweli na haki bila kubagua au kuegemea upande mmoja kwa misingi ya ukabila, nasaba, kiuchumi na hata kisiasa miongoni mwa misingi ingine.

Mafunzo muhimu tunayo pata katika ubeti huu ni ya muhimu katika nyadhifa mbalimbali tunazozichukua. Endapo ni jaji, wakili, mkurugenzi hata mfanzi kazi yeyote yule anastahiki kutenda haki na kutendewa haki bila kudhulumiwa kwa kutotendewa haki na ukweli.

*Shahidi Kuwa wa zuri*

*Hata kwa nduyo sikiri*

*Kikupa fedha johari*

*Ni kheri kutopokea(Ub.27)*

### 4.4.7 UADILIFU

Nadharia ambayo tunaitumia ni ya uadilifu na mbeko. Uadilifu ni hali ya kuwa na maadili mema yanayokubalika na wanajamii wote.

Mtunzi ameguzia haja ya kumtii Rahamani kwa kutojiingiza kwenye maadili hasi, isiyo na mema aliyotusawirishia Mungu. Msanii anamshauri asisuhubiane na marafiki wabaya.

Manufaa ya uadilifu ni mengi kuliko kutoadilika. Mwanadamu kwa njia moja au nyingine huwa na uhasi wa kiwango kidogo. Endapo atashawishika kwa mkondo fulani basi atauzingatia na hivyo kupotosha maisha yake. Yafaa tuadilike katika maisha yetu ili iwe ya manufaa sio kwetu sisi bali ni kwa kila wanadamu wanaotamani maisha ya kiuadilifu.

### 4.4.8 HITIMISHO

*Utendi wa Siiraji* una maudhui na ma funzo ya kiwakati ?Mbinu ya taswira imetufaidi sisi wasomi ikuelewa na kutambua ujumbe ? Haya ni maswali yatakayojibiwa kwenye ukurasa wa mwishoHatuna budi kuiga na kuwasilisha maoni ya mhakikiaaituaye, Munyampala (1965) anaposema kuwa malezi ni kitu cha mbele popote kila mzazi na kuwa watoto bila malezi bora ni shamba lisilo mbolea.

## SURA YA TANO

# 5.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 UTANGULIZI

Uhakiki wetu umechunguza jinsi taswira inavyotumiwa kusuma na kuendeleza maudhui katika *Utendi wa Siiraji*. Katika sura hii tunaazimia kutathmini utafiti wetu kwa njia ya kimuhtasari. Sehemu hii itafaradhi matokeo na madhumuni ya utafiti wetu huku tukilirejeleo ngao zetu hasa nadharia tete, na kujibu suala kuu la utafiti wetu na kana matarajio yetu yametimia kulingana na azimio letu.

Lengo la utafiti wetu lilikuwa kudhibitisha kwamba kigezo cha taswira kina nguvu ya kufanya maudhui na pia ujumbe wa mtunzi ueleweke na utambulike kwa njia ya urahisi na kifasaha kwenye kazi ya kiuandishi ya kifasihi.

Utafiti wetu umelenga matumizi ya taswira kama nguzo mojawapo ya kuvuta hisia za msomaji ili ujumbe ueleweke bila kukisia. Tulihakiki *Utendi* wa *Siiraji.*
Aidha uchunguzi huu umebaini namna taswira imewasilishwa kwenye maudhui ya utungo na msanii kupata nafasi ya kuziteka fikra za msomaji kwa njia urahisi. Kando na maudhui tumetunikiwa na mafunzo muhimu ambayo yalilengwa imfikie mwanawe wala kini imekuwa na itakuwa taa kwa wote watakaopata nafasi ya kuisoma utendi huu hata kama ni wa asili ya Kiamu.

Uchunguzi wetu umeongozwa na nadharia ya maadili. Mihimili mikuu ya nadharia hii ikiwa ni kuadilika kwa mtu binafsi na ushukulio wa jamii kulingana na maadili ya

utimilifu wa mbeko za jamii husika. Kwa mjibu wa nadharia ya maadili, nadharia hii huangalia kazi ya fasihi na uhusiano wake na binadamu hasa maswala ya kimaadili. Kwa kuchagua *Utendi wa Siiraji* ambao ni wa kiwaadhi hatuna shaka tunaposadiki kuwa utafiti wetu utawapa watoto wa jamii yeyote ile kwa kuwapa ushauri wa maisha.

Tumegundua kuwa kwa kudadisi taswira chanya, tumedondoa maudhui mazuri ya kimaadili ambayo ni mojawapo ya muhimili dhabiti ya nadharia tuliyoichagua na kuiangazia.

Kwa hakika nadharia yetu imetufaa na kuchangia pakubwa kutuwezesha kuyapata matakwa ya utafiti wetu.

Katika utafiti wetu, tuliongozwa na nadharia tete zifuatazo.

Kulingana na nadharia ya kwanza, tungependa kutoa hukumu yetu kwamba mtunzi wa Utenzi wa Siiraji Mohammed Kijumwa amefanikiwa katika matumizi ya taswira ambayo ametumia kwa mapana na marefu katika kueneza ujumbe wake.

Aidha tunakubaliana na nadharia tete ya pili kwamba kuziteka makini za wasomaji wa utenzi huu, na hivyo kuufanya maarufu miongoni mwa hadhira yake na hasa wa maeneo ya Lamu.

Kuhusu nadharia ya maadili tumeweza kudhibitisha kwamba, nadharia hii inajitosheleza kutadhmini na kuutafiti utenzi wetu.

## 5.2 MAPENDEKEZO YA UTAFITI

Katika utafiti wetu tumetumia kipengele cha taswira kuchunguza namna mtunzi wa *Utendi wa Siiraji* alivyofanikiwa katika kueneza ujumbe wake. Tungependa kutoa rai kwa watafiti wengine walio na nia na ari ya kuutafiti zaidi wachunguze; Matumizi ya fani katika *Utendi wa Siiraji.*

Ni wazi kutambua kuwa utafiti huu una wajibu mkubwa katika nyanja za fasihi,na umetoa mchango mahsusi katika mwanya uliokuwepo wa uhakiki wa suala la jukumu la taswira kusukuma maudhui ya mtunzi, katika misingi ya nadharia ya maadili na uhakiki utaofuata hauna budi kutumia nadharia hii kwa uhakiki wao.

## MAREJELEO


Abou, Egl, Mohammed (1983) *Life and Works Of Muhammed Kijumwa,* Unpublished PHD, Thesis, SOAS, London.

Allen, V. (1963) *A Catalogue of the Swahili and Arabic Manuscript* in the Library of S.O.A.S England.

Allen, W.T. (1971) Tendi *Six Examples of a Swahili Classical Verse, Form with Translations*. Nairobi, Heinemann

Amin, M..M. (1967) Utenzi wa Uhuru wa Tanganyika, Dar -es-Salaam N.P.C.

Buttner, C. (1892) *Suaheli Schriftstrike in Aiabisechar Scherift,* Lehrbiucher des Seminars fur Orientalicher Sprachen Barlin.

Busaidy (1958) *Ndoa na Talaka*, E.A.E.P (Kenya).

Clara Momanyi (1998) *Matumizi ya Taswira Kama Kielelezo cha Uhalisia Katika Utenzi wa Al-Inkishafi Tasnifu ya Uzamili;* Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Dammann E. (1993) *Afrikanische handhireften* (vol. 1).

Stuttgart.

Desai, S.A.E (1998) *Ta' Lemul Haq Ne* Delhi: Millat Book Centre.

Faisy, S.A.S (1984) *Quran Takatifu*. Nairobi: The Islamic Foundation.

F.E.M K (1988) *Nadharia na Tahakiki,* Dares-Salaam

University Press.

Harries, L. (1962) *Swahili Poetry*, Oxford Clarendom Press.

Harman, W (1986) *A Handbook to Literature.* New York.

Hamondsworht Penguin (1955). Plato. *The Republic*

Hichens, W. (1972) *Al-Inkishafi.* S.A Nasir. Nairobi: Oxford University Press.

Holman, C.H. (1960) *A Handbook to Literature*. New York: Odyssey Press inc.

Hospers J (1978) *Art and Morality: Journal of Comparative Literature* and Aesthetics Vol. No. 1.

*Kenya Constitution 2010* (2008) Review Act

Kezilahabi E (1971) *Rosa Mistika*, E.A.L.B

Kijumwa M. (1927) *Utendi wa Siiraji (1927)*

Kimani N. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi; Nadharia na Mbinu* J.K.F Nairobi

King'ei na Amata, J K (2001) *Taaluma ya Ushairi.* Nairobi: Acacia Stante.

Knappert, J (1967) *Traditional Swahili Poetry*, Leiden London. Macmillan.

Knappert, J. (1967) *A Traditional Swahili Poetry. An investigation Into the Concepts of East African Islam as Reflected in an Utenzi Literature*: Ledien: E.J Brill

Mutiso, K. (1996) *Archetypal Motifs in Swahili Poetry*: Kasida ya Burudani Tasnifu ya PHD chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa bado).

Msokile M. (1993) *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*, E.A.E.P:

Mnyampala M (1965) *Waadhi wa Ushairi* Dares-Salaam, E.A.L.B.

Mbatia M. (2001) *Kamusi ya Fasihi* Nairobi. Standard Textbooks Graphics and Publishing

Msokile, M (1979) *Dhihaka Mume*, Meza Publishing House.

__________ (1952) *Adili na Nduguye* Macmillan.

__________ (1972) *Utenzi wa Via vya Uhuru,* Tanzania Publishing House

_______________ (1983), *Pambazuko* (1983), East Africa Publishing House

___________ (1965) *Diwani ya Muyampala* E.S.L.B NRB Kenya

__________ (1974), *Kichwa maji*, E.X Publishing House.

__________ (1974) *Kichomi.* Nairobi: Heineman.

___________ (1979) *Gamba la Nyoka*, E.A. Publication

__________ (1997) "*Creative Writing in Swahili.*" Makala ya Kongamano la Uandishi wa Kibunifu katika Lugha za Kiafrika SOAS, London.

Mulokozi M.M (1999) *Tenzi Tatu za Kale,* Dares-Salaam: TUKI

Mungania G.B. (1986) *Ushairi wa Mathias Mayampala "Tasnifu ya Uzamili.* Chuo Kikuu cha Nairobi

Mohamed S. A. (1995); *Kunga za Nadharia ya Kiswahili, Riwaya*

*Tamthilia na Hadithi Fupi.* E.A.E.P, NRI
Kenya.

Olali, T. (2008) 6th *Lamu Cultural Festival: Kijumwa Contribution Towards Lamu Wood Carvi*

Saiyyid A. (1972) *Al-in Kishafi: Sauls Awakening O.U.P.* Nairobi, Kenya.

Senkoro F.E. (1987) *Fasihi na Jamii,* Press and Publicity Cen Dar es Salaam, Tanzania.

Shaaban R. (1947) *Pambo la Lugha* O.U.P

Trimingham J.S (1952) *Islam in Ethiopia* London: L Francass.

Tuki (2004) *Kamusi ya Kishwahili.* Toleo La Pili. Ox University

Wafula na Njogu (2007) 2nd Edition, *Nadharia za Uhakiki wa Fas* J.K.F. Nairobi, Kenya

Wallek, R. and Warren, A (1963) *Theory of Literature,* Harmonswoth Publishers.

Wamitila, K.W. (2002) *Uhakiki wa Fasihi (Misingi na Vipengele Vyake).* Phoenix Publishers Nairobi, Ker